

USIZITEGEMEE AKILI

ZAKO MWENYEWE



Na tuendeleo kusimama, kwa muda kidogo sasa, kwa ajili ya maombi. Ni wangapi humu ndani wana haja mioyoni mwao, ambao mngetaka kwamba Mungu angewatendea jambo fulani maalumu kwa ajili yenu katika mkutano huu? Na tumwinamishie vichwa vyetu sasa.

² Baba wa Mbinguni, sisi ni watu waliotunukiwa kukutanika pamoja hapa katika Jina la Bwana Yesu, katika nchi huru ambapo tunaweza kukuabudu kulingana na mwongozo wa dhamira zetu, hata sasa. Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba jambo hili litaendelea kwa muda mrefu. Na sasa jalia kwamba tuyatumie majaliwa haya makubwa tuliyo nayo. Pia jalia kwamba tuweke mioyo yetu yote kwenye ibada hii usiku wa leo, kukuabudu Wewe, ili kwamba iweze kusemwa, ya kwamba, “Mungu alikuwa kati yetu usiku wa leo, akiwabariki watu Wake.” Okoa kila mtu aliyepotea aliye hapa usiku wa leo, Bwana. Na kila aliyerudi nyuma, naomba warudi katika nyumba ya Mungu. Naomba kwa ajili ya kila mgonjwa, na aponywe, wanaoteseke na watembe, na walio vipofu waone, bubu wasikie, shukrani na utukufu vipewe Yesu Kristo kati ya watu Wake. Na ikumbukwe kwa muda mrefu, Bwana, kwa maana tumekutanika pamoja na kuomba baraka hizi katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

³ Kwa namna fulani, katika kuja katika Mkahawa wa Ramada, daima inaonekana kama ni kurudi nyumbani, kwa namna fulani, kwa maana nimekuwa hapa mara nyingi sana hata na—nafikiri hapana budi wameanza kunijua. Nami nafurahia jambo hilo, kwa maana nimepata kundi zuri la watu katika Mkahawa huu wa Ramada. Ule ulio Tucson na huu hapa, wamekuwa wema sana kwetu, kuturuhusu kufanya ibada. Si muda mrefu uliopita, nilikuwa na ibada yangu mwenyewe, kule chini kwenye Mkahawa wa Ramada, na meneja hata hangeniruhusu kugharimia malipo ya jengo hilo. Hilo ni jambo zuri sana. Nitakumbuka jambo hilo ninapoenda huku na huko nchini, pia, sasa, hao wanaowatendea mema watu wa nyumbani Mwake Mungu.

⁴ Sasa tumekuwa, tangu Jumapili usiku, ama Jumapili alasiri, hasa, nyakati nzuri sana katika Bwana, ama angalao mimi nimekuwa nao. Nimekuwa na wakati mzuri sana nikifurahia baraka Zake, na ushirika wa Roho Mtakatifu na wa watu Wake.

⁵ Na—napenda kukumbuka, ya kwamba, sote pamoja tunamwabudu Mungu. Nyinyi ni sifa za Mungu, sehemu ya Mungu, mnapokuwa mwana na binti wa Mungu. Na Mungu yu ndani yako, akitekeleza mapenzi Yake, kama utamruhusu afanye hivyo.

⁶ Kwa hiyo tunatarajia, usiku wa leo, ya kwamba kila mtu atasahau mambo yaliyotukia katika siku zilizopita, na kuweka kila kitu kando, na tuiweke tu mioyo yetu katika ibada sasa; si kwa ajili ya usiku huu tu, bali na katika mkutano ujao. Hapana shaka wajumbe wengi wamekusanyika. Nami kweli niliona baadhi ya hao waliosalia usiku wa leo jukwaani, wakikutanika kwa ajili ya mkutano unaoanza kesho. Nami nawaomba watu ambao wangali wako hapa kwa ajili ya ufufuo ambao ndio kwanza tuwe nao, ya kwamba, kama kweli yawezekana, laiti mngalibaki kwa ajili ya mkutano. Tutakuwa na wahubiri wazuri walio kwenye orodha. Ndugu mmoja hakuweza kuja, na, lakini tunao wengi watakaokuwa hapa kupachukua mahali pake. Nataka kuhudhuria mkutano wote mimi mwenyewe, nipate kuufurahia ushirika huu.

⁷ Mnajua, tunapanda hapa kama wahudumu, na kuhubiri, na daima tunawapa watu kila kitu kilicho ndani yetu. Nilihubiri somo fulani wakati mmoja, mahali ambapo Yesu alisema, “Litafakarini yungiyungi, jinsi hayatendi kazi wala—wala hayasokoti, na hata hivyo nawaambieni hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa kama mojawapo la hayo.” Nami nimepata kujua, yungiyungi halina budi kukua, usiku na mchana, kusokota na kufanya kazi, na kujifanya angavu. Bali halipati baraka kwa jambo hilo, lenyewe. Lenyewe hujifungua, na—na mpitaji anasikia harufu yake nzuri ya manukato. Nyuki hupata asali moja kwa moja toka moyoni. Yeye hutoa kila kitu anachojitahidi kuingiza ndani. Nami niliuita ujumbe wangu, *Kasisi Bwana Yungiyungi*, kwa hiyo hilo kwa namna fulani ni somo la kipekee.

⁸ Lakini—lakini ndivyo ilivyo, wahudumu hujitolea kwa watu, na kwa hiyo ni vizuri kuketi tu na—na kuwasikiza wengine. Ni kama kuota moto, tunapenda kuketi chini ya mwali wa moto wa sisi kwa sisi na kupasha moto mioyo yetu kwa Injili ambayo ndugu zetu wanawahubiria watu. Nami ninafurahia kupata nafasi hii ya kufanya hivyo. Na sasa ninaamini . . .

⁹ Usiku wa leo, Billy aliniambia ya kwamba alisambaza kadi za maombi, zote. Basi hatungeweza kufanyiza msitari wa maombi hapa hata tungefanyaje. Mnaona, ingekubidi kutoka nje upitie kule, na kupitia katika ukumbi wenye giza, kisha uje upande huu. Ungejikwaa kwenye kila kitu, ili kufika hapa. Nao wanaoteseka na viwete wangekuwa katika hali mbaya sana, wakifanya hivyo.

¹⁰ Bali hatujui atakalofanya Bwana wetu. Huenda akaja miongoni mwetu, usiku wa leo, na—na kumponya kila mmoja aliye hapa, kila maradhi. Loo, laiti ningalionga jambo hilo kuliko mistari yote ya maombi niliyopata kufanyiza maishani mwangu, ku—kuona tu mamlaka ya Mungu yakishuka miongoni mwa watoto Wake walio watiifu. Da—daima napenda jambo hilo.

¹¹ Kwa kawaida, kama ukigusana na watu kwa njia yo yote, kama vile kuwawekelea mikono, huenda ikawa, sifikiri wengi sana wangepanya jambo hilo, vema, wangesema, “M—mhudumu fulani aliniwekelea mikono, na, Mungu atukuzwe!” Jambo hilo linawafanya watu wamwangelie mhudumu yule basi.

¹² Bali kama unaweza tu kusimama hapa, uhubiri Neno, na kumwacha Roho Mtakatifu amponye kila mmoja, basi hiyo bila shaka ni neema ya Mungu tu. Ndipo basi Mungu hupata sifa zote, utukufu, na hakuna hata wazo la cho chote kwa ajili ya mtu mwingine. Hivyo ndivyo mimi, katika huduma yangu, sababu ya mimi kutowahudumia wengi sana, isipokuwa . . . Sasa, usiku wa jana, tulijaribu kuwaombea wengi tulivyoweza. Bali kuwawekea mikono . . .

¹³ Kwa kawaida huwa usiku, labda tu kwamba Roho Mtakatifu anakuja miongoni mwetu na kuanza kujidhihirisha Mwenyewe, akijijulisha miongoni mwetu. Ndipo kwa njia hiyo, nafikiri, ni halisi, wakati anapoweza labda katika mamlaka, mnaona. Siwezi kusema sasa, “Mwanamume *huyu*, ama *mwanamke huyu*, ama mtoto *yule*,” mnaona. Roho Mtakatifu anatembea jengoni na kunena na ye yote anayetaka kunena naye. Mnaona, hayo ni mamlaka. Ndipo basi jambo hilo huleta maarifa, kwa maana ni ahadi ya Mungu, na jambo hilo huleta maarifa ya mamlaka ya Mungu, na pia linaleta Uwepo Wake miongoni mwetu. Tungepaswa kuona jambo hilo na kulifurahia! Na haidhuru . . .

¹⁴ Unasema, “Vema, nilikuwa nimepooza mkono. Nilikuwepo hapo usiku uliopita. Si—si—sikupata nafuu kamwe.” Hilo halihusiani nalo hata kidogo. Kwako wewe, yote yamekwisha tayari. Wakati huo huuangalii mkono wako, unaangalia ahadi, unaona. Na kwa hiyo, huwezi ukasema, “Vema, Ndugu *Fulani* hakuomba sala ya imani, ama fulani.” Uwepo wa Bwana ndio uliokupa imani, unaona, kisha Yeye akalituma Neno Lake na kuwaponya.

¹⁵ Sasa, jana usiku ni—nilivunja ahadi yangu tena. Hakika nitajaribu kuitimiza usiku huu, kama nikiweza. Na sasa mtu fulani alisema, “Wewe hukushikilia somo lako jana usiku.” La, si—sikulishikilia; kwa maana, nitawaambieni kwa nini. Nilikuwa nihubiri juu ya somo, hata sasa nasahau lilikuwa ni nini, “*Lakini Mungu Mwingi wa Rehema.*”

¹⁶ Nami nikaingilia kueleza jinsi ambavyo Paulo, akizungumza pale, akasema, “Sisi ambao zamani,” wakati mmoja, wakati mwingine mbali na huu, “tulikuwa wafu katika—katika dhambi

na makosa; ambao Mungu ametuhuisha, akatufanya hai.” Sasa, mnaona, kabla kitu cho chote hakijahuishwa, hapana budi kuwe na kitu pale cha kukihuisha. Hiyo ni kweli.

¹⁷ Kwa hiyo, mnaona, kama Mungu alikuwaja tangu zamani, basi unakuwa sehemu ya Mungu. Na njia pekee unayoweza kuwa mwana wa Mungu ama binti wa Mungu, ilikubidi kuwa sehemu ya Mungu, na Mungu hajakamilika bila wewe. Hana budi kuwa hivyo. Hiyo ni kweli, maana kuna Kimoja tu, chanzo kimoja tu cha Uzima wa Milele, na hicho ni Mungu, na ni Yeye tu aliye na Uzima wa Milele. Mnaona? Naam, nawe ulikuwa sehemu Yake, kiasi kwamba wewe ni sifa, ama katika mawazo Yake hapo mwanzo. Na ya kwamba, kwa kuwa Yeye alikuwazia hapo mwanzo, inasababisha huo mvuto mdogo unaokuelekeza Kwake. Kitu hicho ndicho ambacho hakina budi kuhuishwa. Wengine wao hawatahuishwa kamwe; hawana kitu hicho kweli, hivyo tu.

¹⁸ Ni kama tu vile ungeweka punje ya mahindi ardhini, haikuwa . . . Hata iwe ilikuwa nzuri namna gani, kama haikuwa na mbegu ya uhai ndani yake, haiwezi kuhuishwa kamwe. Bali hivyo mbegu ya uhai haina budi kuwa mle kwanza.

¹⁹ Nami nina ile hadithi ndogo juu ya tai yule, akitembea pamoja na kuku na vifaranga kwa maana alianguliwa na kuzaliwa hapo, bali kamwe hakujisikia kama hao kuku. Basi, mwajua, wakati mamaye alipokaribia pale na kupiga kelele, alisikia sauti ambayo ilikuwa tamu sana kwake, kwa maana, kumbuka, yeye alikuwa tai, kwanza. Ilimbidi tu aje kujitambua, kupata mahali pake.

²⁰ Na hivyo ndivyo alivyo kila mwamini. Wewe hukuzaliwa kwa ajili ya ulimwengu huu. Uliumbwa katika mfano wa Mungu, kuwa mwana wa Mungu. Nawe kwenu si huku kwenye kibanda cha kuku hapa. Wewe ni tai.

²¹ Nanyi mwajua, niliingilia ya huyo “tai” nami sikuweza kuirudisha miguu yangu ardhini, kwa hiyo nilininino tu . . . Niliendelea kwa muda mrefu sana, ndipo nikasahau somo langu lilikuwa juu ya nini, halafu nikapoteza maandishi yangu na kila kitu. Nilikuwa na wakati mzuri sana. Lakini hivyo ndivyo ilivyokuwa, ilikuwa tu juu ya huyo “tai.”

²² Sasa na iwe huyo Tai, Mungu! Mnajua, Mungu huwalinganisha manabii Wake na tai. Naye anajiita Mwenyewe tai; Yeye ni Yehova Tai, Baba Tai.

²³ Na sababu Yake ya kufanya hivyo, tai anaweza kuruka juu sana kuliko ndege ye yote aliyeko, na kwa sababu ameumbwa tofauti na ndege mwingine ye yote. Naam, yeye hajengi kiota chake ardhini kama kuku na kadhalika, bali yeye huruka juu kujenga kiota chake.

²⁴ Na jambo lingine, ni kwamba, yeye ni ndege aliyeumbwa maalum. Sasa kama—kama hajivale, ama kunguru, ama mwewe, ama ndege mwingine yule angejaribu kumfuatilia huko angani,

angevunjikavunjika; yeye hakuumbiwa jambo hilo. Hana budi kuwa mtu maalum kwenda kule juu. Manyoya yake yamekaza sana kuliko ndege mwingine yule.

²⁵ Na—na macho yake yanaona mbali zaidi kuliko ya ndege mwingine ye yote. Na kadiri anavyopaa juu, ndivyo anavyoweza kuona mbali zaidi. Vema, baadhi ya hao ndege, wanaporuka juu wakafikia urefu wanaopaswa kufikia, wao ni vipofu kama popo. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa . . . Vema, wanapoacha kanuni hiyo ya imani, hawajui neno juu Yake basi. “Siku za miujiza zimepita,” kwa nini? Hawawezi kuliona.

²⁶ Bali tai wanaweza kupaa mbinguni, na kwenye mbingu za Mbingu kule juu. Inafaa nini kupaa Huko juu kama huwezi kuona? Loo, ninafurahi sana kuwa mmoja wao, na kushiriki pamoja na kiota kizima chao sasa.

²⁷ Na tufungue Agano la Kale, sasa, katika Kitabu cha Mithali, kilichoandikwa na Sulemani, mmoja wa watu wenye hekima sana duniani, nje ya Bwana wetu Yesu. Bali Yeye hakuwa kabisa kabisa kama Sulemani, kwa kuwa Sulemani alikuwa mtu aliyezaliwa na mwanamke na alizaliwa na baba wa duniani, Daudi. Bali Yesu alikuwa Mwana aliyezaliwa na bikira, na hakuwa mwanadamu kabisa; bali alikuwa Mungu, Mungu-Mwanadamu, Naye alikuwa zaidi ya mwanadamu, alikuwa Mwanadamu na zaidi. Mnaona? Bali Sulemani alikuwa mwanadamu tu kama mimi na wewe, naye akamwomba Mungu hekima, apate kuongoza ufalme wake. Naye alikuwa na karama ya hekima, mtu mwerevu sana tuliyepata kumjua nje ya Bwana wetu. Yeye aliandika Mithali, nami nafikiri ni nzuri sana.

²⁸ Na tutafungua sasa Kitabu cha Mithali, sura ya 1, na, ama sura ya 2, hasa, na aya za kwanza chache za Mithali, ya 2, kuanzia na ya 1. Mithali 2, kuanzia na ya 1, Sulemani anaendelea kuwashauri wanawe, “Mwanangu, kama utapokea . . .” Nasikitika.

²⁹ Nina Mithali 3:1. Samahani. Niliangalia huku katika—katika kitabu changu, nami nikaona kwamba ni Mithali 3 badala ya 1 ama 2. Nasikitika. Mithali 3:1.

Mwanangu, usisahau sheria yangu,

Bali moyo wako uzishike amri zangu.

Maana zitakuwa . . . zitakuongezea wingi wa siku,

Na miaka ya uzima, na amani.

Rehema na kweli zisifarakane nawe;

Zifunge shingoni mwako;

Ziandike kwenye vibao vya moyo wako.

Ndivyo utakapopata kibali na akili nzuri,

Mbele za Mungu na mbele ya mwanadamu.

Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote,

Wala usizitegemee akili zako mwenyewe;

Katika njia zako zote mkiri yeye,

Naye atanyosha mapito yako.

³⁰ Loo, nafikiri hilo ni Andiko zuri sana! Sasa nataka kuchukua fungu, kutoka aya—aya ya 5, *Usizitegemee Akili Zako Mwenyewe*.

³¹ Sasa hili ni fu—fungu la kipekee sana katika siku tunazoishi, kwa maana mkazo leo hakika umewekwa juu ya elimu na juu ya ufahamu wetu wa mambo, siku za—za elimu. Bali tunaona hapa ya kwamba tamshi hili la kipekee, kama ilivyo kwa Maandiko mengine, lina mahali pake, nasi tunatumaini ya kwamba Mungu atatuwezesha kuona mahali hapo ni wapi.

³² Leo sisi huwapeleka watoto wetu shuleni, wapate kupata ufahamu. Ndipo baada ya kumaliza shule ya sekondari, tunawapeleka katika sekondari ya juu wapate ufahamu bora zaidi wa maarifa. Ndipo baada ya kufaulu hapo, baadhi ya hao watoto hubahatika kuingia chuoni, nao wanapitia katika chuo kumaliza elimu yao na ufahamu wao wa maarifa. Yale wanayopata kwa... Mara nyingi, kupata kazi, huna budi kuwa na angaa elimu ya sekondari ya juu, ama elimu ya chuoni, na kadhalika.

³³ Hata hivyo, Sulemani mwenye hekima alitwambia ya kwamba, “tusizitegemee, tusizitegemee akili zetu wenyewe; tusingitegemee mambo haya.” Kwa maana, tunashangaa kwa nini yeye angesema jambo kama hili, kwa maana sababu yake ni kwamba kwa kawaida ufahamu wetu wa kisasa kwa kawaida ni hekima ya mwanadamu, ambayo inapingana na Neno la Mungu. Nami nafikiri hivyo ndivyo Sulemani alivyokuwa akijaribu kuwashauri wanawe, si eti wasisome, bali wasizitegemee akili zao.

³⁴ Nami nafikiri yangekuwa mawaidha mazuri leo, kama tuliwaambia wana wetu na wana wa Mungu, ya kwamba, ni sawa kupata elimu, haina ubaya wote; bali wakati elimu hiyo inapingana na Neno la Mungu, basi tegemea Neno na uachilie mbali elimu yako, unaona, kwa maana Neno. Nayo elimu itadumu na itakupa kazi nzuri, labda sifa njema miongoni mwa wenye kisomo, lakini, hiyo ni sawa, jambo ambalo labda litakuwa na manufaa sana kwako, ikusaidie kifedha na riziki ya—yako, ifanye maisha yawe labda mazuri zaidi.

³⁵ Bali kumbuka jambo moja, mwanangu, huna budi kufa. Haidhuru una elimu jinsi gani, unaweza kujikusanyia ustaarabu kiasi gani, huna budi kuyakabili mauti, kwa maana imeandikwa, ya kwamba, “Mwanadamu hana budi kufa, kisha Hukumu.” Naye Mungu, wakati... Mauti si mabaya sana, bali kuja Hukumuni ndilo jambo baya. Naam, waweza kufa, “bali baada ya huko kufa ni Hukumu.” Naye Mungu hatakuuliza ulipata elimu kiasi gani ulipokuwa humu duniani, ulipata maarifa kiasi

gani, kama ulipata Shahada yako ya Sanaa, ama digrii yo yote uliyopata, hata kama mhudumu. Hutaaulizwa hiyo.

³⁶ Bali utaulizwa, wewe, ulichofanya kuhusu kulifahamu Neno la Mungu. Hicho ndicho kitakachotakikana, kwa sababu Hiyo. Elimu yako ni sawa, bali Neno la Mungu ni Uzima. “Neno Langu ni Uzima,” na kulijua ni Uzima. Naye, Yeye akasema, “Mjue.” Yeye ni Neno. Kwa hiyo unaweza tu kumjua Yeye kwa Neno, kwa maana Yeye ni Neno. Na hiyo ndiyo njia pekee utakayomjulia, ni kwa Neno Lake.

³⁷ Mtu fulani angalikuja na kusema, “*huyu* ni Mungu,” ama “*yule* ni Mungu,” ama “*huyu* ni Mungu,” ama “*hii* ni kweli,” na “*ile* ni kweli,” bali tunarudi kwenye Neno, ambalo ndilo Kweli.

³⁸ Nalo Neno ni kama tu nyo—nyota ya Kaskazini, ni nyota ya kweli. Haidhuru dunia inaelea upande gani, hiyo nyota ya Kaskazini iko katikati ya dunia. Unailekeza dira yako kwenye nyota ya Kaskazini. Daima iko katikati ya dunia. Nyota zingine huelea kila mahali duniani, bali nyota ya Kaskazini haiondoki ilipo.

³⁹ Sasa dira ni Roho Mtakatifu, na (ile) nguzo ya—yako ya kukuelekeza ingekuwa Nyota ya Kaskazini, kwa hiyo Roho Mtakatifu daima ataelekeza kwenye Neno. Roho Mtakatifu hatakuongoza kamwe kwenye kitu kingine cho chote ila kwenye Neno la Mungu. Kwa hiyo mtu angeweza kukubali kanuni ya imani, ambapo inapingana na Neno, halafu ashikilie kusema ana Roho Mtakatifu? Roho Mtakatifu atakuelekeza mbali na hiyo. Inahitaji Roho Mtakatifu kukuelekeza kwenye Neno, kwa maana Yeye ni Neno. Yeye ni Neno, nalo linaweza tu... Kama—kama vile ile sumaku katika dira inaelekezwa tu upande wa Ncha ya Kaskazini, hivyo ndivyo tu inavyoweza kuelekeza. Naye Roho Mtakatifu akiwa ndiye Mbuni na Mwandishi, na Mwenye kulihusha Neno, anaweza kumwelekeza mtu kwenye kitu kingine mbali na Neno?

⁴⁰ Kwa hiyo, wakati mtu anaposema wana Roho Mtakatifu, na kukubali kitu ambacho kinapingana na Neno, inaonyesha kwamba huyo waliye naye si Roho Mtakatifu halisi. Mnaona? Huenda ikawa kweli ni roho, nisingekanusha jambo hilo, bali si—si Roho Mtakatifu wa Kristo. Sasa, mnajua, mara nyingi, wao huchukua roho za wao kwa wao; na kwa hiyo hiyo yaweza ikaelekeza, kama vile katika kundi la watu, kwa kitu fulani, bali haita—haitaelekeza kwa Kristo. Bali Roho Mtakatifu daima huelekeza kwa Kristo, na Kristo ni Neno.

⁴¹ Tunaona jambo hili dhahiri sana katika Biblia. Ama, mimi nalionna. Labda huenda nikakosea, ila, nionavyo mimi, lakini sifikiri hivyo, kwa sababu ya hili, “Usiutegemea ufahamu wako mwenyewe wa mambo.” Kama ukizitegemea akili zako, basi huna budi kwenda kombo. Huwezi kuzitegemea akili za mtu

mwingine, wakati inapofikia Uzima. Kupata Uzima, huna budi kutegemea Neno. Huo ni Uzima.

⁴² Tunaona jambo hili, tangu mwanzo. Limefanywa wazi mno kwetu, tangu mwanzo, ya kwamba Mungu aliipa jamii Yake ya kwanza duniani Neno Lake, kuishi kwalo. Neno Lake tu, ndilo walilipaswa kuishi kwalo. Sasa, hiyo si kwa kula chakula, na kadhalika. Bali walipaswa kuishi kwa Neno Lake, Milele. Na mradi tu walishikilia Neno hilo, waliishi Milele. Lakini fungu dogo la kwanza la hilo Neno lilipowekwa mahali pasipo pake, mfungamano wote ulivunjwa, nayo jamii ya mwanadamu ikatumbukia katika mauti. Mnaona, sasa tunaona.

⁴³ Hawa, ambaye bila shaka alikuwa mtu mwenye akili; wa kwanza kutoka kwa Adamu, aliyekuwa mwa—mwana wa Mungu. Naye Hawa, bila shaka akiwa katika mahali hapo ambapo hapakuwepo na dhambi, hapana mahali pa dhambi, bila shaka lazima alikuwa na wazo zuri sana la jinsi Mungu alivyokuwa. Kwa maana, kila alasiri yeye na mumewe walitembea kwenye utulivu wa bustani, jioni, na kuzungumza uso kwa uso na Mungu. Ni jambo lisilo la—la busara jinsi gani kwamba mtu ambaye angetembea uso kwa uso na Mungu, kila siku, kisha ageukie hoja ya jambo ambalo alilihoji hata akaenda mbali na Neno la Mungu!

⁴⁴ Tungali tunao. Wanahoji kwa wepesi sana hata wakaenda mbali na Neno la Mungu, baada ya kuketi katika Uwepo wa Mungu. Wakiona Neno la Mungu likihubiriwa, Neno la Mungu likidhihirishwa, walevi na wenye dhambi wakija madhabahuni kuongolewa na kufanywa viumbe vipya katika Kristo, watu wenye sifa mbaya wanafanywa mabibi na mabwana; halafu kugeuka kutoka kwenye Kitu hicho kilichobarikiwa kilichowaongoza hadi kwenye Maisha haya, halafu wanapotoshwa kufuata namna fulani ya kanuni ya imani, kupendwa na watu ama—ama waingie kwa kile watakachoita tabaka bora zaidi ya watu.

⁴⁵ Mbona, uko katika tabaka bora sana iliyopo: wana na binti za Mungu. Vema, napenda ushirika huo kuliko vile ningalikuwa pamoja na wafalme wote na watawala, na kila kitu kinginecho. Nipe kundi hilo dogo la watu wanyenyekevu, hata ingawa hawajui tofauti baina ya mkono wao wa kulia na wa kushoto! Mradi tu wanamjua Mungu, na wanampenda na kumtumikia Yeye, hao ndio watu maarufu sana Mbinguni, kwangu mimi. Naam, bwana!

⁴⁶ Sasa, bali tunaona ya kwamba Hawa alishawishiwa kwa urahisi na Shetani, atoke kwenye Neno la Mungu, naye alizitegemea akili zake mwenyewe, kwa maana Shetani alikuwa amemshauri kitu ambacho hakikuambatana na ufahamu wake halisi wa Mungu. Bali alikuwa na jambo jingine aliloambiwa na adui, Shetani, naye akaliadini.

47 Sasa tunapata matokeo ya jambo hili. Lilitumbukiza jamii yote ya mwanadamu mautini, kwa maana mama wa kwanza duniani, alizitegemea akili zake mwenyewe, kinyume cha Neno la Mungu, na kuitumbukiza jamii yote ya mwanadamu mautini. Sasa mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hilo ni Neno. Vema, mwanamke daima ni. . .

48 Kanisa, katika Biblia, linafananishwa na mwanamke. Na kanisa leo linaweza kukubali kundi la mafundisho ya sharti ama kanuni za imani, na kulitumbukiza kusanyiko lote katika utengano na Mungu. Hao watu wanaoyakubali mambo hayo, badala ya Neno la Mungu, ni kama Hawa tu. Na imerudiwa tena na tena, hata imekitumbukiza kizazi hiki chote mbali na Neno la Mungu.

49 Na wakati Neno linapodhihirishwa, Neno linafunuliwa, hawatalikubali, kwa maana hawatafanya hivyo, kwa maana wanazitegemea akili zao wenyewe. “Kanisa hili lilijengwa hapa. Ni mahali pazuri. Ni madhehebu mashuhuri. Ni mshirika wa kundi mashuhuri la watu. Mbona sisi tusiwe washiriki wake? Nitaliamini.” Usiziamini akili zako mwenyewe, bali amini Neno la Mungu!

50 Sasa—sasa iliishia, hatimaye, katika mauti kwa jamii yote, kama nilivyosema, kama ilivyo leo, kwa watu wengi ambao wanazitegemea akili zao wenyewe, mafundisho yao ya sharti na kanuni za imani, na kadhalika, wakidai, “Neno la Mungu si kweli kabisa, kwamba sehemu yake imetiwa pumzi, sehemu nyingine haina pumzi.” Wawezaje kuwa na imani katika Biblia, kama sehemu yake imetiwa pumzi na sehemu nyingine haina pumzi? Kama moja, kama fungu moja si sahihi, basi huenda ikawa yote si sahihi. Yote yapaswa kuwa sahihi, sawa kabisa.

51 Na baadhi ya hizi zinazojiita shule za Biblia, zilizopotoshwa, zinazofundisha maarifa ya mwanadamu, wingi wake, ambapo wao hukutanika na kuketi katika halmashauri ya watu, na kusema, “Sasa angalieni, kama zile siku za miujiza, ziliisha katika siku za mitume.” Na watu wengi chini ya askofu ama watu wenye vyeo vya juu, wangeketi kule na kusema, “Vema, laiti tu ningalikubaliana naye, bila shaka ningekuwa wa pili katika cheo chake.” Mnaona, ndipo unazitegemea akili zako mwenyewe, badala ya kusimamia Neno la Mungu kwa miguu yako miwili. Hilo ndilo linalosababisha mambo haya.

52 Hivi majuzi, mtu fulani. . . Nilikuwa na ubishi juu ya kodi ya mapato. Nao wakaniambia, kasema, “Mbona, wadhamini wako si kitu ila vibaraka, nadhani.”

53 Nikasema, “Kama ningalikuwa na mdhamini katika halmashauri, ambaye alikuwa na wazo tofauti, na hangesimama na (sijali ni nani anazungumzia jambo hilo) na kueleza maoni yake kuhusu jambo hilo, ningemfukuza katika halmashauri hiyo.” Naam, bwana. Hata ingawa yangalikuwa kinyume na

imani yangu, nataka yeye aseme kile anachoamini ni kweli. Hiyo ndiyo sababu nikamweka kule, kuona anayosema juu ya jambo hilo. Bali tuna hayo.

⁵⁴ Angalia, Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 10, “Kondoo Wangu wanaijua sauti Yangu,” mnaona. Sauti, bila shaka, ni Neno Lake, wakati anaponena. “Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu. Sauti Yangu imethibitishwa kwao, kwamba ni kweli. Imethibitishwa kwamba ni Sauti Yangu.” Naam, sasa angalieni, hapaswi kuifuata sauti nyingine. Hawataifuata. “Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu, na mgeni hawatamfuata.” Kwa maneno mengine, hawataelewa sauti ya kitheolojia inayofundisha dhidi ya Neno. Wana-kondoo hawaelewi hiyo kama tu vile yule tai, jana usiku, angeelewa na mlio wa yule kuku. Hauielewi, kwa maana alikuwa tai. Na ni jambo lilo hilo kwa mwana wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili kwelikweli, wao wanafahamu tu mambo yaliyo ya Mungu

⁵⁵ Sasa mtu fulani anasema, “Vema, sasa angalia, ungeweza kufanya *hivi*, nafikiri. Ni, naamini kwamba si *hivi*. Naamini ya kwamba siku za miujiza zimepita. Siamini siku za miujiza zimepita. Siamini ya kwamba huko ni kuponya Kiungu. Siamini *Hili*.” Sasa, Mkristo aliyezaliwa mara ya pili kweli, hayo hayatasimama maskioni mwake, hayaelewi hata kidogo. Basi inawezekanaje mtu anayemwamini Mungu, na anaweza kuisoma Biblia na kujua ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hata akubali jambo kama hilo, sielewi mimi.

Kwa hiyo hao hawazitegemei akili zao wenyewe.

⁵⁶ Ni kama tu vile m—mtoto mchanga. Mchukue mtoto mchanga, hebu azaliwe na umwache wakati mmoja akiegemee kifua cha mamaye, amnyonye, hayo maziwa moto, aegemeze kichwa chake kidogo kifua mwake, ingawa ana umri wa masaa machache tu. Katika siku moja mbili tangu wakati huo, mtoe kwa mamaye umpeleke kifua mwa mama mwingine, atapiga mateke hewani kwa hivyo vijugu na kupiga yowe. Si mamaye. Mnaona, tayari ana kitu fulani kwake, kwa maana yeye ni sehemu ya mama huyu, hata hivyo maumbile yamempa njia ya kumjua mamaye.

⁵⁷ Na kama maumbile yamempa mtoto njia ya kumjua mamaye, kutoka alikozaliwa, ni zaidi sana vipi Yeye amempa mwana wa Mungu aliyezaliwa na Roho wa Mungu. Yeye anamjua Mamaye! Yeye anamjua, kwa sababu alizaliwa kwa Neno, naye analifahamu Neno. Mweke mahali pengine, bila shaka yeye hayuko—hayuko mahali panapofaa, atatoka mle upesi awezavyo. Kwa maana yeye, yeye hazitegemei . . .

Mtu fulani anasema, “Sasa ngoja, mpenzi, huyu ni mama yako sasa.”

⁵⁸ Si mamaye, kwa maana ana njia ya kujua ya kwamba yeye ni sehemu ya mama huyu. Huyu ni mamaye, hakuna mwingine

anayeweza kupachukua mahali pake. Yeye anamjua mamaye. Tazama jinsi—jinsi hivyo ndivyo ilivyo kweli, Mungu amefanya kila kitu kwa jinsi yake.

⁵⁹ Ng'ombe kwa jinsi yao. Mara nyingi katika kuwakusanya, tungelikusanya kundi zima la ng'ombe na ndama wadogo. Nilikuwa hata nashangaa jinsi wangelijua mama zao. Sasa, wao, hao walipokuwa wakishuka milimani, hao ng'ombe wote walichanganyikana. Ng'o—ng'o—ng'ombe aliye na ndama labda ndama mdogo huenda akanyonya kidogo kutoka kwa mama mwingine, kama ana njaa sana; bali tunapowasimamisha, huko mbugani, huyo mama atapita katika kundi la hao ng'ombe na ndama hata atakapompata wake, naye ndama anamkimbilila mamaye. Yeye anajua huo mlio dhahiri katika mlio wake. Naye anamlilia huyo ndama, na mama wengine wanalia mpaka hata huwezi kujisikia ukiwazia, bali huyo ndama mdogo ataupata mlio huo dhahiri wa mamaye, kwa maana yeye ni sehemu ya mamaye.

⁶⁰ Na Mkristo aliyezaliwa mara ya pili kutoka Mbinguni, yeye ni sehemu ya Neno hili. Sawa. Yeye hatamfuata mama mwingine. Yeye ni sehemu ya Neno. Anadumu na Neno. “Kama baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani anayeweza kujifanya tayari kwa vita?” kasema Paulo. Yeye anajua sauti ya Neno. Angalia jinsi hii—jinsi hii ilivyo, mkono wa Mungu uliochaguliwa tangu zamani ukiwafuata kila mahali. Yeye anajua ya kwamba aliamriwa, yeye alikuwa katika Kweli ya Injili. Yeye anajua ya kwamba alizaliwa na Roho wa Mungu. Yeye anajua ya kwamba Roho wa Mungu hawezi kulikana Neno la Mungu, kwa hiyo hatamfuata mgeni. Angalia jinsi. . .

⁶¹ Nilikuwa nikiangalia huku nyuma katika maandishi niliyokuwa nimeandika hapa chini. Ni—niliyapita, bali ikawa kwamba niliona Maandiko ya kusoma, nikafikiri ya kwamba afadhali niyarejee tena. Tazama vile kondoo Wake waliokusudiwa tangu zamani walivyomfuata Yeye, katika siku za wanatheolojia mashuhuri sana tuliopata kuwa nao. Walitoka nje kabisa, kwa maana walimjua. Walijua kile Neno lilikuwa limeahidi kwa ajili ya siku hiyo. Walijua jinsi Masihi atakavyokuwa alipokuja. Ndipo Simoni Petro akamjia, ambaye alikuwa tu “Simoni” wakati huo.

⁶² Naye Andrea alijaribu kumwambia habari zake. “Mtu huyu ni Masihi.” Vema, Simoni, bila shaka, labda alikuwa mkaidi kidogo, naye hangeenda.

⁶³ Bali alipotembea akaingia katika Uwepo wa Yesu, wakati Yesu aliposema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.” Sasa tunajua Yesu aliwaambia mitume Wake ya kwamba aliwajua, naye, “kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Wao walikuwa sifa za mawazo Yake. Kwa hiyo, kwa kuwa hiyo mbegu ilikuwa ndani yake, naye alijua ya kwamba Neno lilisema na

ilikuwa imeahidiwa ya kwamba Masihi angekuwa nabii. Naye alipoona jambo hilo, aliacha kabisa kuvua samaki. Alijua wakati huo kwamba ataacha nyavu zake, kwa maana ange—angeenda awe mvuvi wa watu.

⁶⁴ Kwa maana sasa walisimama wengine waliosimama pale, walioona jambo lile lile likifanywa, na kuliita “pepo mchafu.” Hao walikuwa wanatheolojia, kwa maana halikuwa na ladha ya mafundisho yao ya kitheolojia. Nao wakalikataa, kwa maana walizitegemea akili zao wenyewe, kwa madaktari wao; wakati Yesu Kristo alipokuja katika kutimizwa kwa Neno la ahadi, nao walikuwa vipofu sana hawangeweza kuliona. Wao walitegemea yale makuhani waliyosema, na yale ambayo kanisa lilisema, badala ya juu ya aliyosema Mungu.

⁶⁵ Basi Yesu aliwakemea kwa ajili ya jambo hilo. Yeye alisema, “Yachunguzeni Maandiko, kwa maana mnadai mna Uzima wa Milele ndani Yake. Na hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Maandiko haya ninayowataka myachunguze, yanawaambieni Mimi ni nani.”

⁶⁶ Bali wao hawangetegemea yale Neno liliyosema, bali walitegemea zilivyokuwa akili zao. Wao walizitegemea akili zao wenyewe. Na Maandiko yanatwambia ya kwamba wao walikuwa wametiwa utaji. Utaji wa theolojia zao wenyewe uliwapofusha.

Unasema, “Ndugu Branham, unataka kusema nini?”

⁶⁷ Ninataka kusema hivi. Jambo hilo linatukia tena, hata, wanaume na wanawake na watu watategemea kanisa fulani ambalo wamejiunga nalo na ni washiriki wake, haidhuru Neno la Mungu linasemaje juu yake. Wanaendelea moja kwa moja na jambo hilo, wakizitegemea akili zao wenyewe, na kulipuuza Neno la Mungu, kama kwamba (kamwe) hata halijaandikwa. Ni mbegu isiyo na uhai ya uhai wa binadamu. Ina uhai wa kimwili, bali haina uhai wa kiroho ndani yake kuhuishwa. Utaji ulikuwa juu ya uso wao.

⁶⁸ Angalia sasa, wao walikuwa na mawazo yao wenyewe juu ya vile Mungu anapaswa kuwa, walikuwa na mawazo yao wenyewe juu ya vile Masihi anavyopaswa kuwa. Bali Neno lilisema vile Masihi alivyopaswa kuwa! Naam, mnaona, walikuwa na ufahamu wao wa jinsi angekuwa. Hapana shaka kuhani mkuu alisema, “Makuhani wote walio chini yangu, sasa Masihi ajapo...Sisi tumejenga hekalu kubwa hapa. Tumetenda yote *haya*. Na Biblia ilisema, ‘Yeye atalijilia hekalu Lake ghafla,’ na mambo haya yote. Ajapo, Masihi atakuja papa hapa na kujitambulisha kwetu, na kusema, ‘Mimi ndimi Masihi. Nimewasili. Mimi ndiye Masihi ambaye mmekuwa mkimtazamia.’” Vema, alipokuja, Yeye alikuja kwa njia tofauti sana na vile walidhani itakuwa, wao hawakumtambua. Hawakujua alikuwa Nani. Lakini ninino Yake. . .

69 Na vipi kama mnafiki fulani angaliondoka akaenda pale na kusema, “Mimi ndimi Masihi. Mimi ni Datari *Fulani wa fulani*”? Wao wangelikubali hilo.

70 Bali walipomjia Mtu ambaye alizaliwa kwa uzazi wenye kasoro nyuma Yake, hana elimu ya shule ya yote aliyoenda, kusoma, hakuwa na seminari ya yote, hana kadi ya ushirika; bali alikuwa tafsiri ya Neno la Mungu, lililodhihirishwa. “Kazi, nizifanyazo Mimi, zinawaambia Mimi ni nani. Kama sizitendi kazi nilizoahidiwa nitende, basi msiniamini.”

71 Basi sisi hatuwezi kutumia hili kwa siku hii? Roho Mtakatifu ajapo, ambaye wao wanataka kumweka katika kizazi kingine, wakati Yeye anapokuja katika matendo na madhihirisho ya nguvu Zake za Uzima wa Milele, watu wanataka kuiita “u—ushupavu wa dini ya kishenzi.” Kwa nini? Wao wanazitegemea akili zao wenyewe, wala si Neno la Bwana. Nanyi mnajua jambo hilo ni kweli.

72 Ule utambulisho, ya kwamba fasiri ya Mungu Mwenyewe ni kule kudhihirishwa kwa ahadi.

73 Labda nitasema jambo hilo, kulifanya dhahiri zaidi. Mungu anaponena Neno, Yeye hahitaji mwanamume ye yote ama mwanamke ye yote, ama ye yote yule, kusema Hilo linamaanisha nini. Wakati Yeye aliposema...Vema, unasema, “Mungu alimaanisha *hivi*.” Mungu anamaanisha tu yale anayosema anamaanisha. Mnaona?

74 Sasa Mungu anafasirije Neno Lake Mwenyewe? Kwa kulitimiza. Biblia ilisema, “Bikira atachukua mimba,” yeye akachukua. Hilo halihitaji fasiri ya yote. Mungu alisema, “Iwe Nuru,” ikawa. Hilo halihitaji fasiri ya yote.

75 Mungu alisema, pia, ya kwamba katika siku hizi za mwisho, “Yeye atamwaga Roho Wake juu ya wote wenye mwili,” naye amefanya jambo hilo. Hilo halihitaji fasiri ya yote. Hilo linahitaji tu kukubaliwa, mtu fulani kukubali yale Mungu amefanya. Halihitaji kufasiriwa. Mungu hufasiri Neno Lake Mwenyewe. Mungu aliahidi mambo tunayoona, siku kwa siku, ya kwamba angefanya hivyo katika siku za mwisho.

76 Watu leo, kama ilivyokuwa wakati huo, wanazitegemea akili zao wenyewe. “Mchungaji wangu anasema huo ni ‘ushupavu wa dini.’ Lakini Biblia ilisema ingetendeka. Utategemea akili za nani?

77 Biblia iliahidi katika siku za mwisho, ya kwamba, “Wakati wa Kanisa la Laodikia utakuwa tajiri sana, na uwe unajitoshele...ama kujitosheleza wenyewe, ‘Mimi ni tajiri. Sina haja na kitu. Nimeketi malkia.’” Nalo ni tajiri. Ndipo Yeye akasema, “Wewe hujui ya kwamba una mashaka.” Sasa huo ni wakati mzima wa kanisa, kanisa! “Kwa kanisa la Laodikia, wewe u uchi, kipofu, maskini, mwenye mashaka, na hujui hivyo.” Likiketi juu ya utajiri wake, makumi elfu mara kumi elfu, na

maelfu ya washiriki, utajiri wa ulimwengu mkononi mwake, karibu wote. Wakiuweka wote pamoja, hata leo, kanisa Katoliki na Waprotestanti, wote pamoja, kwa vile wanaungana, wana utajiri wa ulimwengu mzima.

⁷⁸ Tumeofilisika katika taifa hili, karibu kabisa. Tunakopa kutoka kwenye kodi itakayolipwa miaka arobaini tangu sasa, wanavyoniambia, ndivyo walivyosema katika kipindi cha Lifeline. Kodi, tunazotumia sasa, zitalipwa miaka arobaini tangu sasa. Mjukuu wangu mdogo, kama Yesu atakawia, kodi atakayolipa atakapokuwa na umri wa miaka arobaini, ndiyo tunayotumia sasa. Tunatuma misaada nchi za ng'ambo, huku Wahindi wetu na kadhalika wanakufa kwa njaa; tukijaribu kununua ushirika. Hununui ushirika. Humnunui rafiki. La, lakini hivyo ndivyo tunavyofanya. Hivyo ndivyo tulivyo sisi, kuwatoza watu kodi kwa kila wanachoweza kufikia, kodi, kodi, kodi. Nasi hatutamaliza deni letu la vita kwa—kwa mamia ya miaka hata hivyo, nadhani, ambalo tumeingizwa kwake na wanasiasa. Na sasa haitupasi kuwa hivyo. Hakuna sababu ya sisi kuwa namna hiyo.

⁷⁹ Lakini makanisa, yenyewe, yamekuwa tajiri. “Karibu kuufikia utajiri wa ulimwengu,” inasema Biblia, “umo katika kanisa Katoliki.” Hiyo ndiyo sababu Urusi ulilifukuza, sababu ya Urusi kulifukuza. Hicho ndicho chanzo hasa cha ukomunisti, kwa maana kanisa lilifundisha kwamba lenyewe ni kitu fulani, hakuna kilichosalia mahali pengine ulimwenguni.

⁸⁰ Tulipokuwa huko Finland, mvulana huyo mdogo alifufuliwa kutoka kwa wafu. Hao hapo askari wa Kirusi wamesimama wima, nao wakasema, “Tutampokea Mungu anayeweza kuwafufua wafu.”

⁸¹ Tumeunda madhehebu, na mashule na—na mijengo, tukashindwa kufanya aliyotuagiza Yesu kufanya, ilikuwa “Kuihubiri Injili.” Tumejaribu kuuelimisha ulimwengu. Yeye hakusema kamwe, “Uelimisheni ulimwengu; yeye aliye na elimu ataokolewa.” Huna budi kuzaliwa mara ya pili, kujazwa na Roho. Hiyo ndiyo sababu tumeshindwa vibaya sana, kila mahali. Mnaona, tuna mali, tuna kitu chenyeve.

⁸² Sasa nini kitatendeka? Na wakati kanisa hili, Baraza la Makanisa Ulimwenguni, litakapoungana, hamwezi kuona ni nani atakayeongoza? Je! ninyi Wamethodisti na Wapresbiteri hamwezi kuelewa na jambo hilo, ninyi wengine, hata Wapentekoste? Mnasema hamtaingia. Aidha mtaingia ama mtayavunjilia mbali hayo madhehebu. Mtafanya moja ya hayo mawili. Liko mbele yenu kabisa. Hamna budi kufanya hivyo. Ni kulazimishwa, ile alama ya mnyama. Na hivyo ndivyo ilivyo, hasa. Umadhehebu kabisa (naweza kulithibitisha kwa Biblia) ndio ile alama ya mnyama. “Yeye alikuwa kahaba; alikuwa na binti makahaba.” Nasi tunajua ya kwamba hiyo ni Kweli.

Utaratibu wa kidini, unapingana na Neno, na ni mpinga Kristo katika kanuni zake. Si kila kitu kule ni cha upinga Kristo; lakini kwa kanuni zake, taratibu zake ni za upinga Kristo, kwa sababu zinapingana na Neno la Mungu. Kila taratibu za kimadhehebu ndivyo zilivyo.

⁸³ Hayo hapo, mnaona, nawe unazitegemea akili za mtu mwingi-... akili zao, badala ya kuzitegemea akili za Mungu, kwa yale Mungu aliyosema kuhusu jambo hilo. Hiyo ndiyo sababu ni makosa. Vijana ambao wana elimu nzuri huenda katika seminari, wanaenda katika shule hizi za Biblia, kama zinavyoitwa. Na labda wana—wana wito wa Mungu mioyoni mwao. Nao wanaenda kule na wanafunzwa mtazamo mmoja, ya kwamba, “*Fulani* alisema hivyo, Askofu *Fulani*. *Huyu* alisema hivyo. *Yule* alisema hivyo. Halmashauri ya watu ilikubali, iwe *hivi*.”

⁸⁴ Sijali kile asemacho mtu ye yote! Yesu alisema, “Neno la kila mtu liwe uongo, na Langu liwe Kweli. Hata liwe la nani, Langu liwe Kweli!”

⁸⁵ Sasa tunajua Ukweli ni nini? Wakati Biblia inaposema kwamba jambo fulani litatukia, ya kwamba jambo fulani litatendeka, na linatukia hivyo.

⁸⁶ Sasa, Biblia ilisema, “Ndani yake mlipatikana u—utajiri wa ulimwengu; dhahabu, fedha.”

⁸⁷ Sasa kama sisi tuko katika utaratibu wa dhahabu, na tumefilisika, sasa itakuwaje? Itakuwaje? Mnajua, matajiri wa taifa hili, viwanda hivi vikubwa, na watu wa wiski na wa tumbaku, na kadhalika hivyo, hawatastahimili badiliko la fedha, kwa hiyo jambo ambalo litatubidi kufanya ni kuzikopa. Na kuna mahali pamoja tu tunapoweza kuzikopa. Na tutakapofanya hivyo, tutauza haki zetu za wazaliwa wa kwanza kwa kitu hicho. Hiyo ni kweli. Ndipo basi mtafanyaje? Nyinyi ni mali yake, madhehebu hayo. Hakuna jambo lingine mnaloweza kufanya.

⁸⁸ Loo, enyi watu, msifikiri mimi... Huenda mkafikiri mimi nina kichaa. Bali sauti yangu itakaponyamazishwa katika mauti, kanda hizi zitakuwa zikichezwa bado, nanyi mtatambua ya kwamba niliyosema yametimia. Ningekuwa mtu mpumbavu kuliko wote kuchukua msimamo ambao nimechukua, hata dhidi ya kitu hiki, ni—ningekuwa—ningekuwa dhidi ya Mungu, ningepinga kila kitu ambacho ni Mungu, kama mimi (kama nilikuwa) nilikosea katika mawazo yangu na wito wangu. Kitu hicho kingekuwa dhidi ya Mungu. Bali nimechukua msimamo wangu kwa maana naona jambo hilo hapa katika Neno. Ni Neno la Mungu. Kisha naliona likithibitishwa, limehakikishwa kwamba ni Kweli. Hiyo ndiyo tafsiri Mungu anayolipa Neno Lake. Tafsiri ya Mungu ya Neno Lake ni jinsi anavyolithibitisha na kulifanya kweli.

⁸⁹ Kwa nini Mafarisayo hawa walikuwa vipofu? Nini kiliwafanya vipofu namna hiyo? Kwa sababu hawangekubali ufunuo ama thibitisho la Neno.

⁹⁰ Na hiyo ndiyo sababu kwamba makanisa siku hizi ni vipofu, ni kwa sababu hawangekubali ufunuo ambao tayari unathibitishwa. Kama Neno linasema hivyo, na limefunuliwa, halafu linahakikishwa, hata hivyo hawatalikubali.

⁹¹ Hiyo ndiyo sababu hawa Wayahudi, Wayahudi hata siku hizi, hawakubali. Huwezi kuwazungumzia juu ya Kristo, kwa maana ule utaji ungali usoni mwao, wamepofushwa.

⁹² Na kanisa, huwezi kuwazungumzia juu ya Injili yote na nguvu za Mungu, kwa maana mungu wa ulimwengu huu amewapofusha wasione kweli za Mungu, nao wanazitegemea akili zao wenyewe. Wanawake wanapokuja kanisani na kukata nywele zao, kwa maana wachungaji wao huwaambia, “Loo, hilo ni sawa. Mtu huyo ana kichaa.” Bali Biblia ilisema amekosea anapofanya hivyo, Mungu alikataa kuyajibu maombi yake. Na baadhi ya hao wanawake wanaleta fedheha nyingine, na kujaribu kuwa mhubiri, ndipo amefanya jambo hilo maradufu. Biblia ilisema hapaswi kufanya hivyo, hata moja ya hayo. Bali madhehebu ya kanisa watalipokea jambo hilo, na kumchagua na kumtuma kule nje, wakizitegemea akili zao wenyewe!

⁹³ Neno moja la Mungu likiwekwa mahali pasipo pake, ama lisipoeleweka vema, ama lisipokubaliwa, huvunja Mfungamano wote. “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.”

⁹⁴ Mbona kwamba, enyi wanawake, mnanisikia nikihubiri kupinga mambo haya, ya kuvaa kaptura, na rangi, na—na na mitindo hii hapa ya kukata nywele, na upuzi kama huo wote, na halafu kila mwaka ninaporudi mngali katika hali iyo hiyo? Ni kwa sababu mnazitegemea akili zenu wenyewe badala ya Neno la Bwana.

⁹⁵ Basi, enyi wachungaji, mbona msiyasafishe makanisa yenu? Kwa maana mnaienda kanuni yenu ya kimadhehebu badala ya Neno la Bwana. Hiyo ni kweli. Msizitegemea akili zenu wenyewe. Vema, msizitegemea akili zenu wenyewe, bali juu ya Neno la Bwana.

⁹⁶ Hawangelikubali hilo, kwa maana hawangekubali thibitisho. Yesu alikuja na I—Injili, sawasawa kabisa na jinsi tu alivyosema angekuja. Hata mara nyingi . . .

⁹⁷ Yohana alitatanishwa kidogo wakati alipotupwa gerezani, naye—naye akashuka akaenda kule . . . Naye alikuwa amehubiri ya kwamba “Masihi yuaja, Ambaye pepeto Lake lilikuwa mkononi Mwake; Naye atasafisha sana uwanda Wake, na kuyateketeza makapi kwa moto usiozimika, kisha atakusanya ngano ghalani.” Roho wa Mungu akileta, akibubujika Kwake, kama—kama chemchemi. Ndipo basi alipomwona Yesu

amejitokeza, alikuwa maskini Jamaa mnyenyekevu na mpole akisukumwa-sukumwa kila mahali, kila mahali hapa, kwa ajili ya maisha Yake, na upande ule. Mbona, wao hawaku- . . .

⁹⁸ Yohana hakuweza kulifahamu jambo hilo, kwa hiyo akatuma badhi ya wanafunzi wake wakamuulize Yesu kama kweli Yeye alikuwa Ndiye. Ni fedheha jinsi gani kwa Yesu! Baada ya huyo nabii kusimama kule majini, na Neno la Mungu, kasema, “Nilimjua Yeye, kwa maana nilimwona Ro—Roho Mtakatifu, kama hua, Mungu akishuka kutoka Mbinguni kama hua na akaingia ndani Yake, kisha nikasikia Sauti toka Mbinguni, ikisema, ‘Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu,’ kisha Yohana akasema, “Nendeni mkamuulize kama kweli Yeye Ndiye, ama—ama—ama, ‘Tumtazamie mwingine?’”

⁹⁹ Basi Yesu hakumtumia kitabu juu ya jinsi ya kuwa na tabia zuri gerezani, ama ni kanisa gani angalipaswa kuwa amejiunga nalo. Bali Yeye alisema, “Kaeni hapa kidogo mwangalie yatakayotukia, kisha mkamwonyeshe Yohana mambo haya mliyoyaona na kufanywa,” kwa maana kazi Zake alizofanya zilimthibitisha kuwa Masihi, Mwana wa Mungu. “Heri yeye asiye chukizwa Nami.”

¹⁰⁰ Wengi sana wamekwisha chukizwa. Watu wengi sana huchukizwa kwa urahisi sana na Neno la Mungu. Ni—ni kinyume, wanataka kuzitegemea akili zao wenyewe. Hawataki kulichukua Neno la Bwana. Nao hawana budi kwenda jinsi tu wa—wamefundishwa kwenda, na jinsi walivyofundishwa na kile kanisa lao linategemea. Hata kama Mungu aliahidi ya kwamba ange—angefanya inyeshe, kuwe na mvua asubuhi, na kanisa liseme “huo ni upuzi,” wao wangeliamini kanisa badala ya Mungu. Kwa sababu gani? Wao wamezaliwa na kanisa.

¹⁰¹ Lakini mtu aliyezaliwa na Mungu, ni wa mbegu ya Mungu. Na mbegu ya Mungu ni Neno la Mungu, naye huishi tu kwa Hilo. Huo ndio Uzima wake.

¹⁰² Naam, walitegemea akili zao wenyewe, bali hawakutaka kulitegemea Neno la Mungu. Wao walijua vyema zaidi. Ilikuwa katika Maandiko. Waliliita “pepo mchafu,” Mtu huyo. Kwa sababu gani? Kuhani wao alisema, “Mtu ye yote atakayeenda kumsikiza Mtu huyu akihubiri, watatengwa na sinagogi.”

¹⁰³ Wakati mtu mmoja aliponywa ambaye alikuwa kipofu wakati mmoja, na Yesu. Hata wazazi wake, wenye furaha sana kwa sababu ya kuponywa huko, hata hivyo waliogopa kukiri ya kwamba Yesu ndiye aliyefanya hivyo. Naam. Wao walisema . . .

Yeye akasema, “Huyu ni mwanao?”

Kasema, “Ndiyo.”

Kasema, “Ni nani aliyemponya?”

¹⁰⁴ Kasema, “Si—sijui.” Kasema, “Yeye ni mtu mzima, muulizeni. Yeye, yeye anaweza kujisemea mwenyewe.”

¹⁰⁵ Kwa sababu, ilikuwa imesemwa, ya kwamba, “Mtu ye yote atakayezitegemea, akili za Kristo,” badala ya akili zao, “atatengwa na kanisa lao.” Sasa hivi hilo si ni jambo lilo hilo? Nawaulizeni swali dhahiri kabisa. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hiyo ni kweli. Nao wanafanya jambo lile lile. Hata Mungu afanye nini, haina budi iwe ni kulingana na akili zao, si yale Mungu anayothibitisha kuwa ni Kweli. Naam, na basi mtu yule alikuwa na jawabu, hata hivyo.

Akasema, “Uliponywa na nani?”

Yeye akasema, “Mtu mmoja aitwaye Yesu wa Nazareti.”

Kasema, “Yeye ni mwenye dhambi. Hatujui alikotoka.”

¹⁰⁶ Akasema, “Sasa hiyo ni ajabu. Ninyi mnapaswa kuwa ndinyi viongozi wa wakati huu. Na huyu hapa mtu aliyeyafungua macho yangu, jambo ambalo halijatukia tangu ulimwengu ulipoanza, na hata hivyo mnasema hamjui alikotoka Yeye.” Loo, jamani!

¹⁰⁷ Kwa nini? Walikuwa wakizitegemea akili zao badala ya Neno la Bwana. Kwa maana Isaya alisema, “Vipofu wataona, viwete wataruka kama ayala, majangwa yatachanua katika shangwe.” Bali mnaona walizitegemea akili zao wenyewe, si Neno; taratibu zao walizokuwa wameziandaa.

¹⁰⁸ Sasa angalia makanisa ya siku hizi hufanya jambo lile lile. Wameunda jamii kubwa na maalumu ya kiakili, katika taratibu zao za kimadhehebu. Hivyo, wao wana ufahamu maalum sana, hawataki mtu ye yote yule auchezee, mtu ye yote asiingie isipokuwa yeye ni wa kundi hilo.

¹⁰⁹ Msiniambie; naishi Tucson, Arizona. Nilishuka kwenda huko miaka mitatu iliyopita, nikakutana na baraza la makanisa, nami nikasema, “Sikuja kuanzisha kanisa, nimekuja kushiriki pamoja nanyi. Nimekuja kuwasaidieni. Mimi ni mmishenari, mwinjilisti, lo lote nifanyalo.”

Wakasema, “Umekuja hapa kuanzisha kanisa?”

¹¹⁰ Nikasema, “La, bwana. Nimekuja hapa...Kama nikitaka kanisa, nina moja huko Indiana.” Nikasema, “Nimekuja huku kwa sababu Bwana aliniongoza huku katika ono. Nitakaa hapa muda kidogo sasa, isipokuwa aniongoze kwingineko, bali sikuja kuanzisha kanisa. Nimekuja kuwasaidieni enyi ndugu.”

¹¹¹ Hiyo imekuwa miaka mitatu iliyopita. Sijaalikwa kamwe hata mahali pamoja. Kwa nini? Kwa maana kulikuweco na mkutano baada ya jambo hilo, nao wakasema, kama mtu ye yote akinialika mimbarani mwao, wao wangemtenga huyo mhubiri. Mnaona sababu yake? Wakizitegemea akili zao wenyewe!...?...Bila shaka, huo ndio unaoitwa, wao wanatengeneza ufahamu wao maalum.

¹¹² Isipokuwa ujiandikishe katika kitabu chao, umepotea. Mhudumu fulani aliniambia hivyo. “Loo,” mnasema, “huyo alikuwa wa bandia.” Alikuwa Mpentekoste.

¹¹³ Mimi na Jack Moore tuliketi pale tukamsikiza huko Dallas, Texas. Alisema alikuwa, “Atende akaliondoe jina la mtu fulani kwenye kitabu.”

Nikasema, “Kwa nini?”

“Kwa maana yeye alishirikiana nawe.”

Nikasema, “Vema, liondoe.”

Akasema, “Vema, amepotea basi.”

Nikasema, “Ati amepotea?”

“Kwa nini,” akasema, “kama jina lake halimo mle!”

¹¹⁴ Nikasema, “Unataka kusema wewe ni mzee wa jimbo na unaamini jambo hilo?”

Akasema, “Hiyo ni kweli.”

¹¹⁵ Nikasema, “Weka simu chini, bwana. Wewe, wewe. . . Hiyo si neema ya Mungu, hiyo—hiyo, unaona.”

¹¹⁶ “Maana kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, na tunakuwa washiriki wa Mwili huo.” Sijali una alama gani, hiyo haihusiki na jambo hilo. Wewe ni Mkristo kwelikweli kwa kuzaliwa, na hiyo ndiyo njia pekee. Hiyo ndiyo njia pekee uwezayo kuwa; si kwa kujiunga, si kwa kanuni za imani, si kwa kuchochea hili, ama kukariri hili, ama jambo jingine lo lote, wala si kwa elimu, theolojia. Wewe u Mkristo unapozaliwa upya, na huwezi kuzaliwa upya isipokuwa umeteuliwa kuzaliwa upya. “Kwa maana hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, na wote alionipa Baba watakuja.” Amina. “Nitamfufua katika siku ya mwisho.”

¹¹⁷ Hizi wanazoitia shule kuu za Biblia tulizo nazo, wao watasema, wanazitegemea elimu zao wenyewe. Loo, jamani. Wao, haidhuru Neno linasemaje, wao wanaweza kulielezea dhahiri sana, loo, kwao wenyewe, wanajifanya kuamini hayo, na watu wa namna yao kuliadini, ya kwamba, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama nabii, manabii, mitume. Hakuna kitu kama karama za kuponya, na kadhalika. Zote ziliishia katika siku za Biblia.” Wanaweza kujifanya kuamini hayo.

¹¹⁸ Mnajua, Biblia ilisema, “Unaweza ukaadini uongo na ukahukumikiwa kwa huo.” Mnaona, hiyo ni Kweli kabisa. Wao wanaunda, haidhuru Neno la Mungu linasema nini, wao wanazitegemea akili zao wenyewe. Wao, wao wanazitegemea, wanaziamini, wanafikiri ni Kweli. Unaweza kuendelea kuuamini uongo, tena na tena na tena, mpaka unakuwa kwako ni Kweli. Hiyo ni kweli.

119 Lakini tunajua je kama ni Kweli ama la? Mungu alithibitisha kwamba ni Kweli, kwa maana liko katika Neno Lake naye hulithibitisha. Yeye hujifasiria Mwenyewe.

120 Wao wanafanya je, kupata jambo hili? Wanafanya hivyo kwa utamaduni wao, elimu yao, ya ufahamu wao wa di—digrii ya udaktari, na kadhalika, ya kwamba wametoka kwenye seminari fulani na wakajifunza mambo haya.

121 Bali angalieni, enyi marafiki, sikizeni. Hakuna mahali hata pamoja katika Biblia tunatakiwa tufahamu. Hatuombwi kulielewa. Tunaombwa kuliadini. Kuliadini kwa kitu gani? Kwa imani. Kama mnalifahamu, basi hiyo inaibatilisha imani. Huwezi kulielewa, bali unaliadini hata hivyo. Kama ningaliweza kumfahamu Mungu, haingenibidi kumwamini Mungu. Mimi simfahamu Mungu. Hakuna mtu anayemfahamu Mungu. Mimi siwezi kulifahamu Neno la Mungu, bali nalikubali. Naliadini. Sitakiwi kulifahamu.

122 Silifahamu, sikuhudhuria seminari yo yote na ufahamu huu wote wa maarifa ya mwanadamu juu ya Hilo. Mimi najua tu ya kwamba Biblia husema ya Kwamba, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” nami namtumainia katika jinsi iyo hiyo. Najua Yeye aliahidi atakayofanya katika siku hii, nami namtumainia kufanya hivyo naye anafanya. Hiyo ni kweli. Yeye aliahidi neema, niliitafuta hata nikaipokea. Yeye aliahidi kuponya, nami nakuadini na nikakukubali, kisha nikakupokea.

123 Sasa mimi sitaki kuwachelewesha sana, bali nataka kuwaulizeni jambo moja kama mtanivumilia kwa dakika moja, kuwafikiria wale ambao hawakuzitegemea akili zao wenyewe; baadhi ya watu fulani wa Biblia, kwa wachache tu, ambao hawakutegemea akili zao wenyewe, haidhuru ufahamu wa wakati wao ulikuwaje.

124 Hebu tumchukue, kwa mfano, Nuhu. Nuhu aliishi katika siku za utafiti mkuu wa sayansi. Katika siku za Nuhu, labda walijenga mapiramidi, ambayo hawawezi kujenga tena. Sasa hatuna kitu cha kuyajengea, hamna cha kuyainulia majabali hayo kule juu. Hawangaliweza, leo. Siku hizo, walikuwa na dawa ya namna fulani ambayo wangeitia katika rangi na kuzifanya nguo zisichujuke hata siku ya leo. Walikuwa na dawa ya kuhifadhi maiti hata wangeweza kufanya mumiani; hatungeweza kufanya mmoja, leo, hata tufanyaje. Tuna... tumepoteza ustadi mwingi. Siku aliyoshi, katika wakati wa elimu ya kisayansi.

125 Yesu aliutaja, ya kwamba wakati wa namna yiyo hiyo ungerudi tena kabla ya kurudi Kwake, “Kwa maana kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu.” Sasa mtaadini hivyo, sivyo? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Mnaadini ya kwamba Yesu alisema jambo hilo? [“Amina.”] Mnaadini ya kwamba tumekwisha rudi

kwenye wakati huo? [“Amina.”] Sasa, hiyo ni katika Kitabu cha Luka, sura ya 17 na aya ya 29.

¹²⁶ Sasa katika Luka 17:30, Yeye alisema, “Na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, wakati Malaika wa Bwana . . .”

¹²⁷ Naam, alikuwa akisoma Biblia ile ile tunayosoma. Na wakati Yeye . . . Rudi nyuma ukaone ilikuwa siku za namna gani kabla ya mvua ya Nuhu. Rudi nyuma uone ilikuwa siku ya namna gani kabla ya ulimwengu kuharibiwa katika siku za Lutu. Tafuta kujua ilivyokuwa, nawe utaona yale Yesu aliyokuwa akinena habari zake.

¹²⁸ “Katika siku za Nuhu, walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, na kuolewa; hawakujua hata Nuhu alipoingia katika safina, ndipo gharika ikaja, ikawachukua wote.”

¹²⁹ Katika siku za Lutu, kabla tu ulimwengu hauja- . . . moto uliuchoma ulimwengu wa Mataifa, hao watu wa Sodoma, kulikuweco na walawiti, upotovu, kila ghasia ulimwenguni. Ninino kubwa . . . Ilikuwa Los Angeles ya kisasa; si Los Angeles ya kisasa tu, bali Marekani; si Marekani tu, bali ulimwengu. Bila shaka ulikuwa upotovu! Wanadamu walipoteza chanzo chao cha uhai na ufahamu wao wa asili wa akili ya kawaida, wakatoshwa na roho mchafu ambaye alibadilisha utaratibu wao wote wa maisha yao ya kawaida, nao walipagawa na roho wa kipepo. Kama hiyo siyo picha ya siku za Nuhu, sijui, na katika siku za Lutu, namaanisha. Katika siku za Nuhu, pia, kula, kunywa, kuoa, kuolewa, mahakama ya talaka yakijaa, na kila kitu, kama tu vile ilivyokuwa.

¹³⁰ Lakini, kumbuka, kabla ya ulimwengu kuangamizwa, Ibrahimu alitumwa katika uso wa dunia na akapewa ahadi ya mwana. Naye Ibrahimu alikutana na Mungu katika hatua nyingi, kama mfano wa kanisa lilokutana na Mungu. Lakini kabla tu ya yale maangamizi na kurudi kwa yule mwana wa ahadi, ama aliyekuja, hasa, yule mwana aliyekuwameahidiwa, kabla hajaja, Mungu alishuka na kudhihirishwa katika mwili wa binadamu, katika mtu, watu watatu. Nao wakashuka wakaja kwa Lutu; wakaja kwanza kwa Ibrahimu, kisha wakaketi. Ndipo Ibrahimu akabadilishwa jina kutoka Abramam likawa Ibrahimu; Sarai akawa Sara.

¹³¹ Ndipo Mtu huyu, aliyekuwanaazungumza, Elohimu, aliposhuka akaja kuzungumza naye, alisema nini? Alisema, “Yu wapi Sara, mkeo?”

Kasema, “Yumo hemani, nyuma Yako.”

¹³² Kasema, “Nitakurudia wakati uu huu mwakani.” Naye akacheka hemani, nyuma Yake. Ndipo akasema, “Mbona Sara amecheka?” Mnaona? Sasa Yeye angalimuua Sara papo hapo, kwa kulicheka Neno Lake; bali hangaliweza kufanya jambo hilo, kwa maana Sara alikuwa sehemu ya Ibrahimu.

¹³³ Na siku hizi, Yesu alisema katika Luka sura ya 17 na aya ya 30, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, hivyo ndivyo itakavyokuwa wakati wa mwisho wakati Mwana wa Adamu. . .

¹³⁴ Sasa kumbuka, “Mwana wa Adamu” ni *nabii*. Yehova alimwita Ezekiel “Mwana wa Adamu.” Yesu alikuja katika majina matatu: Mwana wa Adamu, Mwana wa Daudi, Mwana wa Mungu. Yeye alijiita “Mwana wa Adamu” ili kwamba watu wafahamu, kwa maana alikuwa yule Nabii ambaye Bwana Mungu angemwinua.

¹³⁵ Sasa angalia, ndipo akaahidi nini? Mwana wa Adamu angejifunua Mwenyewe tena kabla tu ya wakati huo, kabla ya ule moto. Na hiyo ndiyo iliyokuwa ishara ya mwisho aliyoonna Ibrahimu kabla yule mwana wa ahadi kuja; naye akabadilika akawa kijana, naye mkewe akawa kijana mwanamke. Kabla. . . Sasa angalia, Maandiko yanasema hivyo wazi, sasa inatubidi kutarajia hayo.

¹³⁶ Ndipo tukiua ulimwengu uko katika upotovu na mambo yaliyomo ndani yake leo, ukiendelea jinsi unavyofanya, basi twaweza kusema hiyo ni kweli na tusiseme hili lingine ni kweli? Kwa sababu, mtu fulani, unazitegemea akili zao, na si akili za Mfalme wa Uzima ambaye ndiye Mtu yule aliyekuwa pale langoni pamoja nao kule Sodoma. Sasa, tunaona, hatutegemei akili zetu wenyewe.

¹³⁷ Nuhu hakutegemea akili zake. Ulikuwa wakati mkuu wa kisayansi, bali yeye hakutegemea ufahamu wake wa siku zake. Bali alitegemea ahadi ya Mungu, na kuongozwa na nguvu za Mungu, kisha akatayarisha safina kwa ajili ya kuiokoa nyumba yake. Wakati, ilikuwa kinyume kabisa na akili za kawaida; hakukuweko na maji kule juu, hayajakuweko. Bali yeye alijua, kama Mungu alisema yangekuweko, yangekuweko. Kwa hiyo hakuzitegemea akili zake mwenyewe, bali kwa imani aliongozwa na neno la ahadi ya Mungu. Roho alimwongoza, naye akafanya hivyo.

¹³⁸ Ibrahimu, yeye hakutegemea ufahamu wake juu ya maisha ya mwanadamu. Alikuwa amemwoa mkewe akiwa na umri wa yapata miaka kumi na saba. Huyu hapa, mwenye umri wa miaka sabini na mitano, naye mkewe alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano, akiwa mdogo kwa miaka kumi. Bali Ibrahimu hakuzitegemea akili zake, wakati Mungu aliposema kwamba angempa mwana wa kiume kwa Sara. Bali aliita kila kitu, kila thibitisho la sayansi lililokuwa kinyume cha Neno la Mungu, kutegemea cho chote nje ya Neno la Mungu, kama kwamba haikuwa hivyo. Naye akamtukuza Mungu, akatiwa nguvu, akimtukuza Yeye. Hata hakufikiria kuuangalia mwili wake mwenyewe ama hali ya kufa kwa mwili wa Sara, ama—ama mwili wake. Yeye hakufikiria cho chote, bali alitegemea

ahadi ya Mungu. Yeye hakuzitegemea akili zake mwenyewe. Hakuzitegemea hoja zake.

¹³⁹ “Mbona,” unasema, “Ndugu Branham, ni dhahiri kwamba Mungu hangewaponya wagonjwa, tuna madaktari wengi sana walio hodari.”

¹⁴⁰ Biblia ilisema, “Tutupilie mbali hoja.” Tusihoji. Imani haihoji. Imani huamini na kukubali. Angalia.

¹⁴¹ Bali aliamini badala ya kutokuamini; naye akayaita mambo, ambayo hayakuwa, kama kwamba yalikuwa, jambo ambalo lilikuwa kinyume kabisa cha hoja yo yote. Bali yeye hakuhoji. Yeye aliamini tu. Hakuna hoja ambazo zingethibitisha ya kwamba huyo mtoto mchanga angezaliwa. Mwanamke huyo alikuwa ameingia ugumba yapata kama miaka ishirini, na mwili wa huyo mwanamume ulikuwa kama uliokufa. Naye alipokuwa na umri wa miaka mia moja, miaka ishirini na mitano baadaye, yeye bado alikuwa akimsifu Mungu, dhidi ya ufahamu wa namna yo yote. Bali kwa imani, alijua ya kwamba Mungu angetimiza Neno Lake. Yeye hakuzitegemea akili zake mwenyewe.

¹⁴² Vipi kama Musa angalizitegemea akili zake mwenyewe, wakati Mungu alipomwambia ya kwamba ange—angemtoa Farao... ama wana wa Israeli kutoka katika mkono wa Farao? Vipi kama angalizitegemea akili zake mwenyewe, wakati alipokuwa pale karibu na ile Nguzo ya Moto, wakati Mungu aliposema, “Shuka uende kule Nami nitakuwa pamoja Nawe”? Vipi kama alizitegemea akili zake wakati alipowaleta kwenye Bahari ya Shamu, na hao hapo pale majini, na hapa Mungu alikuwa amewaahidi nchi ya ahadi? Vipi kama angalizitegemea akili zake mwenyewe, “Nitavukaje kule? Hatuna wakati wa kujenga daraja. Hili hapa jeshi likija nyuma yetu. Hii hapa milima kila upande. Haya hapa maji mbele yetu, Bahari Shamu”?

¹⁴³ Sasa, kama alikuwa amezitegemea akili zake mwenyewe, angaliitupa mikono yake juu na kutimua mbio, aanguke miguuni mwa Farao, aseme, “Farao, naomba msamaha, nilikosea.”

¹⁴⁴ Bali hakuzitegemea akili zake mwenyewe. Lakini aliomba, kisha Mungu akamwambia asonge mbele, nayo bahari ikafunguka, jambo ambalo lilikuwa dhidi ya hoja zote. Bali yeye hakuzitegemea akili zake mwenyewe.

¹⁴⁵ Vipi kama Yoshua, wakati alipoenda kule na hayo madhehebu mengine kumi, naye akaenda kule na kuona ile nchi iliyoahidiwa na Mungu, naye angalirudi pamoja nao na kusema, “Sasa ngojeni kidogo. Ni kweli. Sisi tulionekana kama panzi. Hao ni majitu. Tunawezaje kuwateka? Hata hatuna panga; ni kile tu tulichookota. Tunawezaje kuingia na kuiteka hiyo nchi? Mbona, haiwezekani kabisa. Hao ni wengi kuliko sisi, watu hamsini kwa mmoja. Wao ni askari waliopewa mazoezi, nasi si kitu ila kundi la wachunga kondoo na wakanyaga matope

kutoka Misri. Inawezekanaje? Hata hatuna ngao na kadhalika, tutawezaje kuiteka?”

¹⁴⁶ Mbona, akili bila shaka zingalithibitisha ya kwamba hawangeweza kufanya jambo hilo. Na mwanajeshi ye yote kama alivyokuwa yeye, ama Musa, hawangaliweza kuzitegemea akili zao wenyewe. Bali akili zao, hawakuzitegemea. Bali walijua ya kwamba Mungu alisema, “Nimewapa nchi hiyo, nendeni mkaitwae!”

¹⁴⁷ Usizitegemea akili zako mwenyewe. Kama ukizitegemea akili zako mwenyewe leo unapokuwa mgonjwa, labda ukiketi kwenye kiti chako cha kusukumia wagonjwa, unakufa kwa kansa, ugonjwa wa moyo, na daktari anasema utakufa, kama ukitegemea ufahamu huo, utakufa. Bali usitegemea ufahamu huo. La hashu.

¹⁴⁸ Vipi kule kwenye kuta za Yeriko, ambako wanasema wangalifanyia mashindano ya mbio za magari juu yake, hizo kuta kubwa mno? Mungu alisema, “Pandeni mwende kule mkazizunguke mara kadha, kisha mkapige baragumu halafu ninyi nyote mpige mayowe, nazo hizo kuta zitaanguka.” Vema, jambo hilo lingekuwa la kipuzi kabisa kwa akili za kimwili. Bali Yohua, akijua jinsi kuta hizo zilivyokuwa nene, kwa maana tayari alikuwa amejenga kuta nyingi kule Misri. Yeye alijua saruji iliyokuwa ndani yake, jinsi zilivyokuwa ngumu, kuweza kustahimili mashindano hayo ya magari kule juu, na hata nyumba zilizojengwa juu yake. Bali yeye hakuzitegemea akili zake mwenyewe. Aliamini yale aliyosema Mungu yalikuwa kweli, naye akalitii Neno Lake, nazo hizo kuta zikaanguka. Bila kuzitegemea akili zake mwenyewe.

¹⁴⁹ Vipi kama yeye alikuwa akipigana hivyo vita, na, kama nilivyokuwa nikihubiri Jumapili iliyopita, na huko jua lilikuwa likitua, adui alikuwa ameshindwa. Usiku huo wangekusanyika pamoja nao wangukuja na jeshi lingine, wawaue watu wake wengi. Sasa vipi kama angalisema, “Nahitaji mwangaza wa mchana. Sina budi kupata mwangaza zaidi wa jua. Vema, sasa ngoja kidogo. Mungu aliweka utaratibu huu, na jinsi jua linavyozunguka ndivyo ulimwengu unavyozunguka. Sasa hebu tuone, kama ningesema jua lisiname. . . Labda nao ulimwengu utasimama sasa, ndipo utapoteza nguvu zake za uvutano, nitaanguka?”

¹⁵⁰ Yeye hakuzisikiza akili zake. Jambo alilosema tu, lilikuwa, “Wewe jua, simama kimya; na, wewe mwezi, usitoke ulipo,” nalo likamtii. Yeye hakutegemea akili zake mwenyewe. Bali alitegemea ahadi ya Mungu, “Nimekupa wewe nchi hiyo; nenda kaitwae.”

¹⁵¹ Yeye amekupa ahadi ya Roho Mtakatifu. Unaweza kumpata katika mkutano huu. Unaweza kumpata sasa.

152 Usitegemee, “Unajua, mimi nimechoka. Nakwambia, nimekula chakula kingi sana cha jioni. Ni—ni—ningechukia Yohana jamani! nikifanya jambo hili.” Loo, jamani! Unazitegemea akili zako mwenyewe.

153 “Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wale wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

154 “Daktari alisema nitakufa. Alinifanyia uchunguzi, kisha akasema nilikuwa na hii kansa, na nilikuwa na *hii*, au cho chote kile. Sina budi kufa.” Usitegemee ufahamu huo. Mungu ni Mungu Bwana wako Ambaye huyaponya magonjwa yako yote. Kwa hiyo usitegemee ufahamu huo, usizitegemee akili za mwanadamu. Zitegemeeni akili za Mungu.

155 Vipi kuhusu Samsoni, kule uwanjani, wakati Wafilisti, watu elfu moja walipomvamia? Na hicho hapo kimesimama, maskini kijitu chenye nywele za kipilipili, kirefu *hivi*. Hakufanya hivyo; vema, yeye hakuwa stadi wa kutumia upanga, kwa maana hakuja; hakuwa amefunzwa, mafunzo ya kijeshi. Yeye alikuwa mwenye nywele za kipilipili, kama mwanamke, mwenye vishungi saba vilivyoning’inia chini, mvulana wa mamaye, amesimama pale, na hawa hapa Wafilisti elfu moja wanakuja. Vema, hakuwa na kitu mkononi. Akaangalia chini, akaona mfupa wa kale wa taya la nyumbu uliochomwa na jua hata ukawa mweupe, naye akauchukua.

156 Sasa kasema, “Hebu tuone sasa, sitafanya mengi kwa *hii*, kwa maana hizo chapeo zao vichwani mwao ni . . . Hao Wafilisti, hao askari wote, wote wana mikuki. Wote wana dereya za chuma. Na vyepeo vyao vina uzito wa pauni kumi na tano kila kimoja, watu wakubwa mno, wote wametoka. Vema, kama ningalipiga kwa mfupa huu mwepesi wa taya la nyumbu, moja ya hivyo vyepeo, naam, ungalivunjika vipandevipande. Hivyo tu?”

157 Yeye hakuzitegemea akili zake. Yeye alichukua tu kilichokuwa mkononi mwake, akaanza kuwapiga hao Wafilisti. Na baada ya kuwaangusha chini kwa kuwapiga elfu moja wa hao, bado angali alikuwa na huo mfupa wa taya mkononi mwake. Amina.

158 Sijali theolojia ya mwanadamu inasemaje, usitegemee. Litegemee Neno la Mungu, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Bila shaka, yeye aliamini.

159 Vipi kama Daudi angalimsikiza Samsoni . . . theolojia ya Sauli? Huyu hapo amesimama Goliathi anajigamba kwelikweli, na kila mtu anaogopa; Sauli, mkubwa kuliko jeshi lote tangu mabega hadi kichwani. Goliathi akasema, “Mtu mmoja aje apigane nami. Hakuna haja ya—ya sisi wote kufa. Kama nikikuua, basi nyote mtatutumikia. Na kama ukiniwa, naam, tutawatumikia,” maana alikuwa na uwezekano wa kumshinda.

Hivyo ndivyo ibilisi anapenda kufanya, wakati ameileta seminari yake yote, na hao wote, wakati anapokuja, mnaona.

¹⁶⁰ Maskini Daudi mdogo alikuwa akitembea pale, amevaa kipande cha ngozi ya kondoo; mwekundu, ameinama mabega, jamaa mdogo mwenye uzito wa kama ratili mia moja, mia moja na kumi. Akasema, “Unataka kuniambia ya kwamba majeshi ya Mungu aliye hai, ambayo yametahiriwa kwa agano, yatasimama pale na kumwacha huyo Mfilisti asiyetahiriwa ayadharau majeshi ya Mungu aliye hai?”

¹⁶¹ Sauli akasema, “Njoo hapa, kijana.” Akasema, “Napenda ujasiri wako, bali siku za miujiza zimepita. Hatuna mambo kama hayo, mnaona. Na hebu niwaambie jambo fulani, unaweza kuonyesha kadi gani ya ushirika, mnaona? Hata huna chapeo. Huna kitu ila kombeo mkononi mwako. Mnaona? Huna Ph.D. ama LL.D. Utawezaje kufanya jambo hili? Mbona, mtu huyo ni shujaa wa vita. Mbona, yeye—yeye amehitimu D.D, L maradufu, Ph.D., LL.Q. Mbona, yeye ana digrii nyingi sana, angeweza kuzibandika akajaza ukuta kwazo. Nawe u nani? Mchungu kondoo.”

¹⁶² Akasema, “Lakini ninataka kukwambia jambo fulani.” Akasema, “Unajua nini?” Kasema, “Nilikuwa ninachunga kondoo za baba yangu kule nje, ndipo,” kasema, “simba akaja akamshika mmoja, na kukimbia. Basi wajua, nilichukua kombeo hili dogo nikamfuatilia, nikamwangusha. Nikamtwaa mwa—mwana-kondoo kutoka kinywani mwake, naye akanishambulia nilipofanya hivyo. Nikachukua tu kisu nikamuua.” Kasema, “Nikarudi. Na huyu hapa dubu anaingia, anamfukuza huyo kondoo, akamnyakua na kukimbia. Nikamuua, pia.” Akasema, “Sasa Mungu... Si Ph.D. yangu, si akili zangu mwenyewe. Siwezi kukwambia jinsi ninavyofanya jambo hilo. Sijui linavyofanywa. Bali yule Mungu,” amina, “yule Mungu aliyeniokoa na makucha ya dubu na simba, ni zaidi vipi ataniokoa katika mikono ya Mfilisti yule asiyetahiriwa!”

¹⁶³ Askofu, Sauli, alisema, “Unajua, naamini una wito, kijana. Ngoja nikwambie, kama ungekuja huku, nitakufundisha jinsi ya kupigana na mtu, unaona. Nami nakwambia, mimi—mimi ni daktari, kwa hiyo vaa chapeo yangu. Nataka kukuvalisha.” Daudi akasimama pale, nao wakampachika Ph.D., LL.D., na yote hayo, na—na maskini jamaa huyo mdogo hangeweza hata kusogea. Hakuja jinsi ya kufanya hivyo.

¹⁶⁴ Akasema, “Sijajaribu hili. Vazi hilo la kidini halinikai mimi. Nivueni kitu hiki. Acheni niende na kile Mungu alichonifanikisha nacho.” Na hicho kilikuwa ni imani katika nguvu za Mungu. Na—naye hakuzitegemea akili zake mwenyewe. Yeye hakutegemea kile alichosema mtu mwingine. Alitegemea imani. Kwa sababu, alijua kama Mungu alikuwa

amemwokoia katika makucha ya dubu, si Yeye atazaidi sana kumwokoia na Mfilisti huyo!

¹⁶⁵ Vema, kama Mungu alikupenda vya kutosha kukutoa katika dhambi na kukujaza na Roho Mtakatifu, imekuwaje kwenu enyi maskini wanyonge msio na uti wa mgongo mliopo kila mahali nchini, si Yeye atawaokoa zaidi sana na mateso yenu wakati Yeye aliahidi atafanya hivyo? Neno la Mungu lilisema hivyo. Yeye atafanya hivyo. Bila shaka, Yeye alimtoa katika huo mkono.

¹⁶⁶ Loo, kila mmoja wa manabii, vipi kama wangezitegemea akili zao katika nyakati zao? Hawangeenda kamwe mbele za makuhani wao na makuhani wakuu, na kuwaita “kuta zilizopakwa chokaa” na kila kitu. Hawangaliweza kutabiri dhidi yao. Wangukuwa kama baadhi ya hao manabii wa kisasa, wangukubaliana nao, wavae mavazi mazuri, na wawe katika nyumba za wafalme.

¹⁶⁷ Vipi kama Yohana angelijaribu kuzitegemea akili zake mwenyewe? Bali yeye aliondoka akaenda kule.

¹⁶⁸ Walisema, “Naam, ngoja kidogo, Yohana, usihubiri juu ya *Ndoa na Talaka*.”

¹⁶⁹ Yeye alienda mbele ya mfalme Herode, akasema, “Si halali kwako kumchukua.” Naam, bwana.

Kasema, “Vema, unajua huyo ni nani? Huyo ni . . . ? . . .”

“Sijali huyo ni nani.” Yeye hakuzitegemea.

¹⁷⁰ Kasema, “Sasa unajua huna mengi. Uko chini hapa katika jangwa hili. Shirika halitakupokea, kama ukiendelea kutenda mambo kama hayo.” Yeye hakujali juu ya shirika lo lote. Yeye hakuzitegemea akili zake mwenyewe, bali kwa akili Zake Mungu. Bila shaka.

¹⁷¹ Kuna mtu mmoja ambaye alizitegemea akili zake mwenyewe, na jina lake lilikuwa Yuda Iskariote. Loo, yeye. . . Si—sioni jinsi yeye angelifanya jambo hilo. Yeye alikuwa ametembea uso kwa uso na Kristo, kama tu Hawa alivyofanya hapo mwanzo. Alikwishaona thibitisho, alikuwa amemwangalia Mungu usoni, kama alivyofanya Hawa wakati wa jua kupunga. Hawa alimwangalia Kristo, wakati wa jua kupunga, bustanini. Naye Yuda alikuwa ameketi wakati wa jua kupunga, katika bustani ya Gethsemane na mahali pengi, naye alikuwa amemwangalia Kristo yule yule; alikuwa amemsikia akifundisha, akijithibitisha Mwenyewe kwa Neno, akathibitishwa kuwa Ndiye nabii ambaye Musa alikuwa amenena kwamba angeondokeshwa. Naye akawaambia Yeye alikuwa Nani katika Maandiko, na mambo yote juu yake. Walikuwa wameliona likithibitishwa na Mungu, ya kwamba Yeye alikuwa ndiye, halafu yeye akazitegemea akili zake mwenyewe.

¹⁷² Yeye angeweza kufanya jambo hilo? Ni kwa sababu hakuwa nalo hapa ndani kamwe, kwanza. Yeye hakuwa mbegu iliyo na uhai. Alikuwa mwana wa upotevu, aliyezaliwa kutoka upotevu, akarudi katika upotevu. Sasa tunaona. Bali akatoka akaenda, na labda huenda yeye alikuwa na wazo la akili yake. Huenda alifikiri ya kwamba Yesu . . . Alimheshimu sana, “Sasa, mwajua, huenda nikamuza kwa vipande thelathini vya fedha. Na kama nikifanya hivyo, nitapata fedha, nami naweza kufanya jambo fulani nazo. Naye anaweza kujiokoa.” Mnaona, hakujuua, katika Maandiko, ya kwamba Yeye aliondokesha kupachukua mahali pale pale.

¹⁷³ Wala watu leo hawatambui hali waliyo nayo. Imekusudiwa kwamba kanisa hili la Laodikia liwe katika hali hii, kumweka Kristo nje. Naye anagonga mlango, akijaribu kuingia, [Ndugu Branham anagonga mara tano mimbarani—Mh.], hakuna kuungwa mkono mahali po pote, hata hivyo. Akithibitisha Neno Lake siku hii ya leo, kama alivyofanya kila siku, nao wanaondoka wanaliacha. Wakizitegemea akili zao, hiyo—hiyo tu.

¹⁷⁴ Ama, labda, hebu na tuseme haya ambayo—ambayo aliwazia. Labda kama alimuza Kristo kwa vipande thelathini vya fedha, mbona, kwamba angepata ku—kushirikiana na baadhi ya madhehebu makubwa ya siku hizo, Mafarisayo na Masadukayo. Yeye angesema, “Sasa ngoja, Yeye anaweza kujishughulikia. Nimemwona katika vita vikali; na—najua ya—ya kwamba anaweza kujishughulikia. Kwa hiyo huenda nikapata fedha, namna fulani ya kustaaafu ku—kudogo, kama ilivyokuwa. Halafu, tena, naweza kuwa na sifa nzuri miongoni mwa makanisa haya leo, kama nikimsaliti kwao.” Mnaona? Bali yeye alizitegemea akili zake mwenyewe, badala ya ufahamu kwamba hilo lilikuwa Neno la Mungu lililothibitishwa, naye akamfanyia Yesu yale hasa Maandiko yalisema angefanya.

¹⁷⁵ Na, leo, ulimwengu wa kanisa umemfukuza Kristo katika siku hizi za mwisho, kama tu vile Kitabu cha Ufunuo kilisema wangefanya. Ni roho ya Yuda tena, katika mfano wa kanisa, “Wakiwa na mfano wa utauwa, bali wakilikana Neno.” Mnaona? Hiyo ni kweli. Sasa, loo, jamani, matokeo yake yalikuwa nini? Mauti, kama tu yalivyompata Hawa. Na ndivyo yanavyowapata wale wengine wote wanaojaribu kulipotosha Neno la Mungu. Na kuzitegemea akili zao wenyewe. Hata sasa hivi wanauza, si kwa vipande thelathini vya fedha, bali labda wanakuwa, loo, afisa fulani mkubwa, ujuzi fulani wa seminari. Hauna thamani ya vipande thelathini vya fedha, bali wanauza tu hata hivyo; wanauza ufahamu wao wa Mungu, nje, kwa kitu kama hicho.

¹⁷⁶ Ni tofauti jinsi gani na yule Mtakatifu mkuu Paulo, aliyekuwa na elimu yote angaliweza kujivunia. Bali yeye alisema, “Nimekikataa kitu hicho chote, cha hoja zangu, kabisa. Nilikutana na ile Nguzo ya Moto siku moja, nikiwa barabarani

nikienda zangu Dameski.” Ndipo akasema, “Sikuja kwenu kwa ufasaha wa maneno, kwa kuwa, kama ningefanya hivyo, ninyi m—mngetumainia hekima ya wanadamu. Bali nilikuja kwenu katika nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu, ili kwamba mkategemee Neno la Mungu.” Amina. Kasema, “Kama Malaika kutoka Mbinguni akiya, akihubiri kitu kingine cho chote, na alaaniwe,” Wagalatia 1:8. Hiyo ni kweli. La, bwana. Yeye hakufanya hivyo.

¹⁷⁷ Maskini yule mwanamke kisimani, yeye alikuwa mzinifu. Bali alijua ya kwamba makanisa yalikuwa yamemtupa nje. Na, bali yeye hakuzitegemea kamwe akili zake mwenyewe. Alipokutana na Huyu pale kisimani, aliyemwambia dhambi zote alizokuwa amefanya, alikimbia mjini. Sasa haikuwa sawa kwa mwanamke kufanya jambo hilo, kuingia mle na kusema cho chote, kwa maana alikuwa kahaba. Bali baada ya kukutana na Yesu, yeye hakuzitegemea akili za watu, wa siku hizo. Alikuwa, kasema, “Njoooni, mmwone Mtu aliyeniambia mambo niliyotenda. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?” Yeye hakuzitegemea akili zake. La.

¹⁷⁸ Bikira Mariamu, wakati Malaika Gabrieli alipokutana naye na kumwambia ya kwamba atapata mtoto, bila ya kumjua mwanamume. Whiu! Halijatukia. Yeye hakuzitegemea akili zake mwenyewe, ya kwamba mwanamke hangeweza kumpata mtoto bila ya—ya mume. Yeye hakutegemea hizo. Bali alisema, “Tazama mjakazi wa Bwana, na iwe kwangu kulingana na Neno Lako.” Yeye hakusema, “Mimi nitafanyaje hayo? Na nitafanya lini hayo? Na yote yatatukiaje?”

¹⁷⁹ Yule Malaika alisema, “Roho Mtakatifu atakujilia juu yako kama uvuli; na Kitu hicho Kitakatifu kitakachozaliwa kwako kitaitwa Mwana wa Mungu.”

¹⁸⁰ Akasema, “Tazama mjakazi wa Bwana.” Yeye hakuchukua hoja yake, aseme haiwezekani. Yeye alisema tu, “Tazama mjakazi wa Bwana.” Hiyo ni kweli. Tazama.

¹⁸¹ Yule—yule mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu, daktari alimwambia, kasema, “Hakuna matumaini.” Yeye alikuwa tayari ametumia mapato yake yote, na waganga, na hakuna hata mmoja wao aliyeweza kumsaidia. Naye hakutegemea hilo. Wakati Yesu . . . Yeye alipita katikati ya umati wa watu, na yule mwanamke akasema, “Naamini kama nikiligusa vazi la Mtu yule, nitapata afya.” Basi akaenda kule.

¹⁸² “Sasa ngoja, daktari alisema, ‘Huwezi kupata afya.’” Alikuwa na huku kutokwa na wa damu kwa miaka kadha wa kadha. Alizidi kuwa mdhaifu wakati wote, akawa mahututi. Madaktari walikuwa wamemkatia tamaa. Hayo ndiyo maarifa yote waliyokuwa nayo.

¹⁸³ Lakini yule mwanamke akasema, kwa imani! Hakuna Maandiko yanayomwambia afanye hivyo. Bali akasema, “Kama

nikigusa upindo wa vazi lake, nitapata afya,” naye akajipenyeza karibu akamgusa. Akarudi, akaketi chini.

¹⁸⁴ Ndipo Yesu akageuka akasema, “Ni nani aliyenigusa?” Akaangalia kila mahali mpaka akampata. Akamwambia juu ya mtoko wake wa damu.

¹⁸⁵ Naye akahisi wakati huo, mwilini mwake mwenyewe. Hangelithibitisha jambo hilo wakati huo, bali alihisi mwilini mwake mwenyewe wakati huo ya kwamba kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma. Yeye hakutoa hoja, “Kama daktari alikuwa amemkatalia, kitu kingine cho chote kingemsaidiaje?” Yeye hakuanza kutoa hoja, bali alishikilia imani.

¹⁸⁶ Sasa Biblia ilisema, “Ya kwamba Yeye ndiye Kuhani Mkuu, leo, anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Usianze kuhoji, kusema, loo, hiyo ni . . . Yeye alisema, “Leo ndivyo alivyo Yeye. Yeye sasa hivi ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu. Yeye yule jana, leo, na hata milele!”

¹⁸⁷ Mnafikirije nilipokuwa kule kama mhubiri wa Kibatisti, naye Malaika wa Bwana akakutana nami kule na kuniagiza niende nikafanye mambo haya ninayofanya? Mbona, mchungaji wangu alisema, “Wewe una kichaa. Mbona, umekuwa na jinamizi, wewe.”

Nikasema, “Afadhali uchukue kadi yangu ya ushirika sasa hivi.”

¹⁸⁸ Sasa, yeye alisema, “Wawezaje, na huku hata huna elimu ya sekondari, kuhubiri ulimwenguni kote? Wawezaje kuwaombea wafalme na watawala, na hata hu—hu—huwezi kutumia sarufi yako vizuri.”

¹⁸⁹ Mimi sikuwa nikitumainia sarufi yangu. Sikuwa nikitumainia uwezo wo wote niliokuwa nao. Niliagizwa. Haleluya! Nami sikuanza kuhoji. Na kama ningekuwa nimesikiza hoja, labda maelfu ya watu wangelikufa, miaka mingi iliyopita. Bali niliuchukua Ujumbe jinsi hasa alivyosema, huku na huko ulimwenguni.

¹⁹⁰ Nami ninaenda tena, kwa neema ya Mungu; si kwa hoja, bali kwa agizo. Haleluya. Mimi sikutegemea. . . Mnasema, “Wewe una umri wa miaka hamsini na mitano.” Kama ningalikuwa na tisini na mitano, hilo halimaanishi kitu. Yeye yungali Mungu yeye yule aliyekuwa pamoja na Ibrahimu. Naam, bwana. Usizitegemee akili zako mwenyewe.

¹⁹¹ Na baada ya ile ishara kutokea, huku Sauti inafuata, na makanisa yakaanza kunikataa na kufunga milango yao, juu ya Fundisho, hata mtu ye yote kati yao hawezi kuthubutu kusimama mbele yangu kusema ni kweli ama ni uongo. Namsai mtu ye yote kati yao. A-ha. Si kuwa mwerevu, bali ninajua nilipo.

Hiyo ni kweli. Walifanya nini? Walifanya nini? Wanafunga kila mlango. “Sasa utafanyaje?”

¹⁹² Juzijuzi, juu ya mlima, nilikuwa nimesimama pale. Nikasema, “Bwana, nina mlango mmoja uliofunguliwa katika taifa zima, ni juavyo mimi, nao ni huko Phoenix, Arizona. Ndio tu nilio nao.” Nami nikaanza kushuka mlimani. Dhahiri kama nilivyowahi kumsikia mtu ye yote akinena, kasema, “Hiyo ni nini kwako? Wewe nifuate Mimi.” Si akili zangu tena. Nitategemea ahadi Yake.

¹⁹³ Loo, rafiki, usitegemee hoja. Ndipo unapaza sauti pamoja na Eddie Perronet wa kale:

Nyote lisifuni Jina la Yesu!
Malaika na wamsujudu;
Ileteni taji ya kifalme,
Ndipo mkamvike taji Mfalme wa wote;
Mkamvike taji Mfalme wa wote.

¹⁹⁴ Hiyo ni kweli. Usitegemee yale unayofikiria, yale mtu mwingine anayofikiria. Kwa imani ikubali ahadi ya Mungu. Utafanya jambo hilo? Sasa si ati kama mtu mwingine alifanya hivyo, kama hawakufanya jambo hilo, lakini na wewe je? Utamtendeaje huyu Yesu aitwaye Kristo, ambaye anajifunua siku hii, vile vile jinsi alivyofanya Yeye siku ile? Mnamwamini Yeye? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Na tuombe.

¹⁹⁵ Bwana Yesu, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana, Mungu wa miungu, Mungu wa watawala wote; wa Kwanza, wa Mwisho; Alpha, Omega; Mwanzo na Mwisho; Nyota ya Asubuhi yenye Kung’aa, Waridi la Uwandani, Nyinyoro ya Bondeni, Shina na Mzao wa Daudi; njoo, Bwana Mungu, yeye yule jana, leo na hata milele!

¹⁹⁶ Ubariki umati huu wa watu, Bwana. Huu . . . [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] tunajitayarisha kuanza kesho. Tumekuwa na mkutano mdogo hapa, nawe umetubariki kwake. Umejifunua Mwenyewe kwetu. Naomba, Mungu, ya kwamba utaendelea kujifunua Mwenyewe kwetu. Tubariki usiku wa leo. Tusaidie. Sisi ni watu wahitaji.

¹⁹⁷ Pia, Bwana, Wewe unajua sitaki kuwakemea watu, bali nawezaje kunyamazisha huo mwako mtakatifu? Sipendi kufanya jambo hilo, Bwana. Unayajua maisha yangu, moyo wangu. Sina budi kufanya jambo hilo. Nami naomba, Mungu, ya kwamba Wewe utanisaidia kufanya jambo hilo. Nipe neema tu, na usiniache nitegemee akili zangu, bali hebu nitegemee ahadi Yako. Katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁹⁸ Nawatakeni, kila mmoja, mwe na kicho sana kwa dakika chache tu. Katika umati huu wa watu, kuna wanawake wengi na wanaume wanaoketi hapa, hapana shaka, walio wagonjwa. Ni

wangapi wagonjwa na wanaoteseka hapa, inueni mikono yenu, mseme tu, “Namhitaji Mungu”? Inua mkono wako sasa hivi, “Ninamhitaji Mungu.”

¹⁹⁹ Sasa, siwajui watu wengi sana. Nawajua wavulana hawa watatu wanaoketi papa hapa. Namjua Bw. Dauch na mkewe wanaoketi pale. Nafikiri, nafikiri huyu ni Dada Moore. Sina hakika. Sivyo, Dada Moore? Mbali na hao, nafikiri hakuna wengine. Ndugu Mike, na jukwaa. Hao ndio, nionavyo mimi, ninaowajua.

²⁰⁰ Lakini Baba wa Mbinguni aliyeahidi, na katika siku hii Yeye angejithibitisha Mwenyewe katika kizazi hiki, jinsi hasa alivyofanya kule Sodoma. Yeye aliahidi jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Alijidhihirisha Mwenyewe! Mnaamini jambo hilo? [“Amina.”]

²⁰¹ Sasa kama mtaomba, na kwa imani! Sasa msijaribu kuhoji, “Naweza kumgusa kama Kuhani Mkuu?”

²⁰² Sasa, Biblia ilisema, Agano Jipya, “Yeye ni Kuhani Mkuu sasa hivi. Yeye anadumu Kuhani Mkuu mithili ya Melkizedeki. Yeye ni Kuhani Mkuu milele. Hakuna Kuhani Mkuu mwingine ila Yeye. Hakuna mpatanishi mwingine kati ya Mungu na mwanadamu, bali Mwanadamu Kristo.” Hiyo ni kweli. Yeye Ndiye Pekee, Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

²⁰³ Sasa kama Yeye anadumu Kuhani Mkuu yeye yule, nayo Biblia ilisema, “Tunaweza kumgusa kwa mambo yetu ya udhaifu,” kama vile maskini mwanamke yule alivyofanya aliyegusa vazi Lake, imani yako inaweza kumgusa usiku wa leo naye atatenda vile vile, katika mwili wa kibinadamu, kama alivyofanya wakati alipokuwa katika mwili wa kibinadamu kule kwenye—kwenye mwaloni wa Ibrahimu. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye aliahidi atafanya hivyo. Sasa ombeni tu, mtu ye yote aliye na haja. Nami—nami. . .

²⁰⁴ Ni kama vile nilivyosema, karama si kama vile ati unachukua kisu, na kama unataka kukata *hiki* nacho, unaweza kukikata; ama ukate *hiki*, unaweza kukikata, ama cho chote unachotaka. Hiyo si karama ya Mungu. Mnaona? La.

²⁰⁵ Karama ya Mungu ni njia uliyo nayo ya kujiondoa njiani. Na karama na miito vimekusudiwa na Mungu tangu zamani. “Karama na miito hata havina majuto.” Unazaliwa nazo. Ngia ndogo unayojitia ndani yake, bali huwezi kukanyaga pedali. Mnaona? Mungu hana budi kuiendesha. Huna budi kujiondoa njiani.

²⁰⁶ Imani yako inaweza kuiendesha, si yangu; yako. Yangu huiondoa tu njiani. Wewe amini kwa moyo wako wote ya kwamba Yesu Kristo yu hai leo.

²⁰⁷ Usizitegemee akili zako, unasema, “Vema, sasa angalia, mi—mimi niko katika hali ya taabani, ndugu. Hunijui

mimi. Nimekuwa katika kiti hiki cha kusukumia wagonjwa. Nimekuwa . . .”

²⁰⁸ Sijali umekuwa nini, na uone kama Mungu hatashuka na kufanya yale aliyofanya hasa alipokuwa humu duniani katika mwili wa kawaida. Yeye atafanya hivyo katika mwili wako, katika mwili wangu, pamoja kama kitu kimoja tukimwamini Yeye. Yeye atafanya hivyo kwa sababu aliahidi atafanya hivyo.

²⁰⁹ Sasa usitegemee yale mtu mwingine anasema, “Loo, hiyo—hiyo ni kuwasiliani kimawazo,” kama wanavyokuita. Kasema Yesu alikuwa kitu kile kile. Walisema alikuwa mpiga ramli, “pepo.” Bali Yeye alikuwa Mwana wa Mungu, kwa maana alikuwa kulingana na ahadi ya Mungu.

²¹⁰ Sasa, kama nilivyosema, ma—mahali petu, haitubidi kuwa na hayo, kuja na kuwawekelea watu mikono. Tuliwawekelea mikono jana usiku. Bali kitu tu kinachokupasa kuwa nacho ni imani, kisha utambue. Kwa imani unalikubali, kwa imani. Si—si cho chote ambacho . . .

Usiseme, “Vema, sasa inaweza kutendwa namna gani?”

²¹¹ Kama ningeweza kuwaambia jinsi ilivyofanywa, basi haingekuwa imani tena. Sijui inavyofanywa. Sijui, bali naamini. Si—sijui jinsi—jinsi Mungu anavyomwoko mwenye dhambi, bali anamwoko. Sijui jinsi Mungu anavyofanya yo yote ya mambo haya, bali nayakubali. Yeye, Yeye huyafanya, na hiyo ndiyo njia. Kwa maana, siwezi kuielezea. Sasa, vema, mimi . . . Hayataelezewa kamwe. Hamna mtu awezaye. Kwa maana, kama ukifanya hivyo, basi si imani tena.

²¹² Sioni jinsi Mungu na Kristo wangeweza kuwa Mtu yule yule, bali walikuwa hivyo. Maandiko yalisema. Vema, huwezi kuielezea, bali walikuwa hivyo. “Baba Yangu yu ndani Yangu. Si Mimi ninayezitenda kazi; ni Baba Yangu ndani Yangu. Kama sizitendi zile kazi Zake, basi hiyo inaonyesha Mimi si Wake. Bali kama nikizitenda zile kazi Zake, basi Yeye anashuhudia Mwenyewe ya kwamba Mimi ni Wake.”

²¹³ Vema, ni jambo lile lile leo, jambo lile lile hasa. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kama utaamini.

²¹⁴ Sasa kuna mtu aliyeketi papa hapa mbele yangu, yuna nywele nyeusi. Ana saa mkononi mwake, suti nyeusi. Amevalia miwani. Kama mnaweza kuangalia moja kwa moja, mnaweza kumwona ameketi huku amefunga macho, anaomba. Simjui mtu huyo. Baba wa Mbinguni anajua simjui. Bali nitamwangalia kwa dakika moja tu, kwa maana anaonekana kama kwamba yeye ni mwaminifu sana, akiketi pale. Tangu nilipomtaja, huyo mtu alifunga tu macho yake akaanza kuomba. Mtu huyo ni mgeni kwangu, hiyo ni kusema, kwa mikono yangu. Simjui. Mungu anamjua mtu huyo, Naye anaweza kunifunulia. Kama ahadi hiyo ni kweli katika Biblia, anaweza kunifunulia kwa nini mtu huyo

amefunga macho yake, na kile anachoombea. Mnaamini hivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²¹⁵ Unaamini hilo, bwana? Tafadhali fungua macho yako, unaketi papa hapa, angalia papa hapa. Unaamini jambo hilo? Sawa. Sasa unajua sikujui. Sisi ni wageni sisi kwa sisi. Bali Mungu anakujua. Sasa yeye alianza kulia, analia. Kwa maana, naweza kumwambia sasa ya kwamba Mungu atatimiza haja yake, mnaona, kwa maana hiyo ndiyo iliyomgusa wakati huo, hiyo Nuru; kutoka gizani, ikageuka ikawa Nuru. Mnaona?

²¹⁶ Sasa, huyo mtu, anamwombea mtu mwingine, na huyo ni mvulana huyu mdogo anayeketi upande huu karibu naye. Huyo ni mwanawe. Hiyo ni kweli. Sasa, huyo mvulana mdogo anaumwa na—na amechafukiwa na tumbo, na pia michango yake ina kasoro. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

²¹⁷ Hutoki hapa. Hutoki Arizona. Umetoka California. Hiyo ni kweli. Nawe ni mhudumu, na unashiriki na Assemblies of God. Hiyo ni kweli. Kasisi McKeiger . . . Ama, Kasisi Keig, hiyo ni kweli. Sivyo? Punga mkono wako namna *hii*. Sasa mvulana wako atapata afya. Imani yako!

²¹⁸ Sasa nini? Sasa kuna mtu aliyeuinua mkono wake, yeye haniujui, mimi simjui. Bali ilikuwa nini? Yeye alimgusa Kuhani Mkuu. Sasa, mnaona, Yeye hangeweza kuzitegemea akili zake mwenyewe. Sasa yale anayopaswa kufanya, sasa yeye anafanya nini sasa? Hana budi kuamini ya kwamba yale aliyoambiwa, ni kweli, maana anajua yeye haniujui. Hiyo ni kweli.

²¹⁹ Hapa, hapa anaketi mwanamke ameketi papa hapa mbele yangu, pia, ameinamisha kichwa chake. Yeye anaugua kansa. Yeye pia anatoka California. Natumainia hatakosa jambo hili. Bi Adams, hilo ndilo jina lako. Mimi sijapata kumwona maishani mwangu. Naam, hiyo ni kweli.

²²⁰ Kuna bibi anayeketi huku nyuma upande *huu*. Siwezi kuweka mkono wangu juu yake, bali naona Nuru imening’inia juu yake. Yeye ana shida nyingi sana. Ana shida na shingo yake, kwanza. Na jambo jingine, yeye—yeye ana matatatizo ya kiroho ambayo yanamsumbua. Pia ana shida za nyumbani; binti yake ndiyo kwanza atoroke. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, sivyo? Ameuinua mkono wake. Bibi Miller, hiyo ni kweli. Unaamini? Mungu atamrudisha, atauponya mwili wako. Sasa, sijapata kumwona maishani mwangu. Yeye ni mgeni kabisa.

²²¹ Kuna bibi anayeketi hapa mkutanoni. Yeye—yeye hatoki hapa, yeye pia ametoka California. Ana kansa, na hiyo kansa iko kwenye titi lake. Yeye amefanyiwa upasuaji, titi moja, nayo ikahamia kwenye hilo lingine. Hiyo ni kweli. Bibi wa Kalin, hiyo ni kweli. Unaamini Mungu atakupata afya? Sawa, unaamini. Mimi ni mgeni kwako, bibi. Sikujui. Hiyo ni kweli, mnaona, yeye ni mgeni.

Mpate kujua ya kwamba Mungu yuko hapa!

222 Kuna bibi anayeketi karibu kabisa naye. Jina lake ni Bibi Harris. Yeye ni mgeni kabisa kwangu. Bali wakati Roho alipomgusa mwanamke huyu, yeye pia anamhurumia. Naye anatoka California. Hiyo ni kweli. Naye ana shida ya bega lake. Hiyo ni kweli. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako kusudi watu waweze kuuona; mgeni kabisa.

223 Usizitegemee akili zako mwenyewe. Ni nini kinachoweza kufanya jambo hilo? Huwezi kueleza jambo hilo. Hicho ni kitendawili. Halielezeki. Waulize watu hao; sijawaona kamwe maishani mwangu, kamwe sikujua neno juu yao. Ingeweza kuendelea tu mkutanoni.

224 Lakini, sasa angalia, usizitegemee akili zako mwenyewe. Bali tegemea kile alichohidi, ya kwamba yeye angefanya jambo hilo; kama huyo si Roho yeye yule aliyekuwa akikaa katika mwili wa kibinadamu, ambaye alijua ya kwamba Sara alicheka hemani, nyuma ya huyo Mtu. Hiyo ni kweli? Naye aliahidi, kabla tu ulimwengu haujaangamizwa kwa moto, wakati Mwana wa Adamu angejifunua tena katika njia ile ile, kama Mwa—Mwana wa Adamu (kinabii) angejifunua Mwenyewe katika mwili wa kibinadamu kama alivyo hapa pamoja nasi usiku wa leo, kama alivyofanya wakati huo. Sasa tunaishi wakati gani? Karibu tu na yale maangamizi.

225 Rafiki, usisimame hapa ndani, tena, ukiwa mwenye dhambi. Mkubali Yesu Kristo wakati ungali katika Uwepo Wake. Sasa, najua, kwa kawaida wahudumu wamezoea kushawishi na kusimulia hadithi, juu ya mama ambaye amekufa na ameondoka. Hiyo ni sawa. Bali hatuji juu ya msingi wa mama zetu waliokufa. Mama yangu amekufa, pia; baba yangu, pia. Bali tunakuja, kwa ufahamu, tukikubali juu ya msingi wa Mungu akijidhihirisha Mwenyewe katika Kristo Yesu, kuzichukua dhambi za ulimwengu. Tunakuja na kuamini juu ya ule Upatanisho. Na wakati amelithibitisha Neno Lake. . .

226 Sijali umehudhuria kanisa gani, Methodisti, Batisti, Katoliki, Presbiteri, ama huna kanisa kabisa. Kama utakubali ya kwamba umelifahamu vinginevyo, na unajua ya kwamba kweli hujazaliwa mara ya pili kweli, lakini unataka kuzaliwa, na unataka kuikubali sasa, ile ahadi sasa. Huenda usijazwe sasa, bali utajazwa wakati. . . wakati mikutano inaendelea. Unataka kuikubali juu ya msingi huo, tafadhali simama kwa miguu yako nipate kukuomba papo hapo unaposimama. Kila mmoja humu ndani anayejua. . .

227 Usizitegemee zako, “Loo, jamani, nilinena kwa lugha.” Sasa, hilo halina uhusiano wo wote nalo. Mimi naamini katika kunena kwa lugha, pia.

228 Bali nimewaona wachawi, pepo, na kila kitu, wakinena kwa lugha na kufasiri hayo. Hiyo ni kweli. Waulize wamishenari

huku chini, tunaweza kujua, Ndugu Creech, nawe unajua ya kwamba hilo ni kweli. Nimewaona wakinena kwa lugha, na kunywa damu kwa fuvu la kichwa cha mwanadamu, wakimwita ibilisi. Bila shaka. Nimewaona wakiweka penseli chini, nayo ingeinuka na kuandika katika lugha, zisizojulikana; naye huyo mchawi, mlozi anasimama pale, anazifasiri.

²²⁹ Kwa hiyo kunena kwa lugha si ishara ya kwamba una Roho Mtakatifu. Kama hiyo, kama ukinena kwa lugha na kukana Neno hili, kuna kasoro mahali fulani. Sawa, a-ha, sawa. Usizitegemee akili zako mwenyewe.

²³⁰ Mtu fulani sasa, unasema, “Vema, nilipiga kelele.” Na mimi pia hufanya pia. Bali usitegemee jambo hilo.

²³¹ Nimeona namna zote za nguvu za pepo zikipiga makelele na mayowe. Nimewaona Waislamu wakipiga makelele na mayowe hata, wanajichochea sana hata, wangejichoma mikono kwa vibanzi. Huko India, nimewaona wao wakipiga mayowe na kurukaruka, wakachukua mipira ya maji, yenye kulabu, na kuisukumiza ngozini mwao na kutembea juu ya makaa ya moto, sawa, huku wanamkana Yesu Kristo.

²³² Mnaona, usizitegemee akili zako mwenyewe, bali juu ya Neno la Mungu. Kama maisha yako hayaambatani na Biblia hii, kuamini kila Neno lililo mle; nawe unataka kuliadini, nawe unataka Mungu kufanya mapenzi Yake kupitia kwako, kwa maana unaweza kuwa sehemu ya Mungu, tafadhali simama na useme, “Nitaikubali sasa hivi, ndugu.” Asante. Asante. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Vizuri sana. Mungu akubariki. Mungu na awakirimie, hawa wote walio waaminifu. Mnasema . . . Endeeleni tu—tu kusimama, hebu tu . . .

²³³ Unasema, “Mimi ni mshiriki wa kanisa, Ndugu Branham, bali mimi hasa ni Mpentekoste; bali wakati kweli inafikia kusema kweli mimi naweza kuamini Neno hilo lote ni Kweli, siwezi tu kufanya jambo hilo, bali na—nataka kufanya hivyo. Nisaidie, niombe. Nataka kusimama na kusema, si—simaanishi kusema tutaketi hapa, ama, nita—nitashuhudia katika kanisa hili, ya kwamba nilikuwa hivyo.” Lakini wajua, katika kilindi cha moyo wako, sivyo ulivyo. Mungu anajua sivyo ulivyo, pia, unaona, kwa hiyo mbona usisimame tu. Usizitegemee akili zako mwenyewe, bali litegemee Neno Lake.

²³⁴ Mtasimama, wengine zaidi? Mtu mwingine ye yote anayetaka kusimama? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe. “Mungu, nisaidie.” Mungu awabariki. Hilo ni zuri. Endeeleni kusimama.

²³⁵ Wasema, “Hilo litanifaa kitu?” Simama wakati mmoja, uone kama itakufaa. Ulitilie maanani kabisa, “Nataka, Ndugu Branham, nataka kuwa sahihi. Nataka kuwa sahihi.”

236 Naam, mimi sisemi uliache kanisa lako. La, bwana. Kaa papo hapo ulipo, wewe uwe tu mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu kabisa katika kanisa hilo. Unasema, “Vema, sijui atakayosema mchungaji wangu.” Yeye atakufurahia kama umejazwa, kama yeye ni mtu wa Mungu. Unaona hiyo ni kweli.

237 “Nuru yenu na iangaze mbele ya watu wapate kuyaona matendo yenu mema wamtukuze Baba yao.”

238 Mungu akubariki. Vema, Mungu awabariki nyote wawili, na wewe; na wewe, ndugu, wewe. Mungu awabariki, kila mmoja. Mungu akubariki. Mungu akubariki wewe hapa chini.

239 Sasa ninyi mliosimama, kama mnajisikia vizuri zaidi juu yake baada ya kusimama, inueni mikono yenu mpate kuwaambia wengine ya kwamba mnajisikia vizuri zaidi juu yake baada ya kusimama. Mnaona, kila mkono. Mnaona? Bila shaka, mnajisikia vizuri zaidi. Mnaona, ninyi ni waaminifu. Mnasimama, kusema, “Nitakuwa shahidi.”

240 “Yeye atakayenitetea Mimi huku, Nitamtetea kule. Yeye atakayenionea haya Mimi hapa mbele ya hawa watu, Mimi nitamwonea haya mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu.” Usizitegemee hoja zako mwenyewe. Litegemee Neno la Mungu. “Yeye atakayenikiri mbele za watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu.”

241 Kutakuwa na wengine, kabla tu hatujaomba? Na tuviinamishe vichwa vyetu basi. Mungu akubariki, dada. Kweli. Mungu akubariki, na wewe, ndugu. Bila shaka. Kwaweza kuwa na mwingine ye yote, wakati tu vichwa vyetu vimeinamishwa? Mungu akubariki, wewe. Naam, hiyo ni sawa, mngali mnasimama. Tutangojea tu muda kidogo, muda kidogo tu. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Wasema, “Ina maana yo yote, kusema, ‘Mungu akubariki?’” Hiyo ni kutamka baraka zangu kwenu. Mungu akubariki.

242 Baadhi yenu mnaosimama ukutani, ambako hamna nafasi ya kuketi, mwaweza kuinua mikono yenu, mseme, “Mimi, Mungu, ni mimi?” Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, na wewe; na wewe, dada; na wewe, ndugu yangu; na wewe, dada yangu.

243 Loo, Roho Mtakatifu anatembea vizuri juu ya mkutano. Mnaweza kumhisi Huyu? Mungu akubariki, ewe kijana mwanamume hapa jukwaani. Mungu akubariki, huko pembeni. Mungu akubariki, ewe jamaa mdogo. Naam.

244 Ee Roho Mtakatifu, tembea upya mioyoni mwetu sasa. Tuonyeshe makosa yetu, Bwana. Tuta- . . . hatutazitegemea akili zetu wenyewe, hoja zetu wenyewe. Bali tutakutegemea Wewe, kwa maana tunajua ya kwamba tunasimama katika ahadi Yako ya Kiungu, ya siku hizi iliyothibitishwa. Wewe umejifunua kupita, kupita hoja yo yote. Hatungeweza kuhoji wala kuieleza. Bali Wewe umeshuka ukaja hapa miongoni mwetu sasa, na

kutujulisha ya kwamba Wewe uko hapa, na wanaume na wanawake wanaamini jambo hilo na kulikubali.

²⁴⁵ Mungu, mchukue kila mmoja wetu ukamweke kifuani Mwako, na uwafiche katika Mwamba wenye Imara hata mioto itakapopita. Tuko karibu kuchomwa moto, Bwana. Tunajua jambo hilo. Tumerudi Sodoma. “Bali wenye haki hawataangamia pamoja na wenye hatia.” Wewe utawaita watoto Wako, Bwana. Ulimwambia Lutu, “Ondoka hapo. Ondoka.” Naomba, Mungu, ya kwamba kila mmoja aliye katika hali hiyo usiku wa leo, aliye huko nje, ambao hawana uhakika wanakosimama. . .

²⁴⁶ Mungu, wao hawangethubutu kushuka kwenda katika barabara ya njia moja, njia mbaya. Hawangeweza kuvuka penye taa nyekundu kwa kubahatisha, kama wao wana akili timamu, kwa maana huenda wakauawa. Basi mtu anawezaje kubahatisha juu ya kikomo chao cha Milele, kukisia tu, kuthubutu, kujasiria bila ruhusa halisi ya kujasiria, ati kwa maana wao ni washiriki wa kanisa ama madhehebu? Na kwa kweli hawawezi, hawawezi kufahamu jinsi ambavyo Neno la Mungu laweza kuwa leo kama lilivyokuwa wakati ule, jinsi ahadi hizi zinavyoweza kudhihirishwa. “Wakati wa mitume umepita.” Wasaidie, Baba. Nawakabidhi Kwako katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁴⁷ Asante, ndugu yangu, dada. Nina furaha sana kukuita ndugu yangu, dada.

²⁴⁸ Kumbukeni, Mungu atanifanya niwajibike kwa kila neno, kwenye Siku ya Hukumu. Kila nilichohubiri usiku wa leo, sina budi kuwajibika kwake. Ninafahamu jambo hilo. Yale nimefanya tangu nilipokuwa kijana mdogo, kuhubiri Injili hii, kisha nitupwe nje?

²⁴⁹ Sasa ni wangapi wenu walio wagonjwa na wanaoteseka, hapa usiku wa leo, nanyi mnataka kuombewa? Inueni mikono yenu. Sasa, mwaweza kunifanyia jambo jingine moja? Wekeaneni mikono mmoja juu ya mwingine. Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi. Kila mtu ainamishe kichwa chake sasa, kama tu kwamba ulikuwa kanisani, huku jukwaani.

²⁵⁰ Mungu mpendwa, katika Jina la Yesu Kristo, na kwa Uwepo Wake, Uwepo uliothibitishwa! Neno lile lile ambalo limekwisha hubiriwa, limethibitisha ya kwamba ni wewe yule jana, leo, na hata milele. Naomba Roho Mtakatifu apitie juu ya kundi hili la watu sasa hivi. Wengi wao wamekuja na kukukubali Wewe kama Mwokozi wao, wengi waliorudi nyuma wamekukubali Wewe na wakarudi. Ee Mungu, naomba kwamba katika Jina Yesu Kristo, ya kwamba utamponya kila mtu. Wewe ulisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Wewe uliahidi jambo hilo, Bwana, na watoto waaminio wameweka mikono yao mmoja juu ya mwingine.

²⁵¹ Shetani, umeshindwa. Watoke watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo. Waachilie watu hao waende zao, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, katika Jina la Yesu. Amina.

²⁵² Wote wanaoamini ya kwamba Yesu Kristo sasa ni mponya wenu, na pia Mwokozi wenu, na mnataka kumkubali juu ya misingi iyo hiyo, simameni kwa miguu yenu, mkaseme, “Sasa namkubali Yesu Kristo kama mponya wangu, na pia Mwokozi wangu.” Vizuri sana! Bwana asifiwe! Mungu ashukuriwe! Sasa hebu tuinue mikono yetu tukamwimbie.

Nitamsifu, nitamsifu,
Nimsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;
Mpeni sifa, enyi watu wote,
Kwa maana Damu Yake imeosha kila taka.

²⁵³ Loo, je! hamjisikii vizuri? Pungeni mikono yenu. Loo, jamani! Hebu na tuuimbe tena.

Nitamsifu, nitamsifu,
Nimsifu Mwana-Kondoo kwa . . . (Kumbukeni,
“yeye yule jana, leo, na hata milele,” ndivyo
alivyo huyo Mwana-Kondoo.)
Mpeni sifa, enyi watu wote,
Kwa maana Damu Yake imeosha kila taka.

²⁵⁴ Mnaupenda huo? [Kusanayiko linapaza sauti, “Haleluya! —Mh.] Hebu tunyoshe mikono yetu na kupeana mikono na mtu fulani. Huu ndio mwisho wa mkutano, ulioanza katika huu mkutano. Sema, “Mungu akubariki, ndugu, msafiri. Mungu akubariki.” Hilo ni sawa. Hilo ni jema. Vizuri sana! Sasa mnaamini tutakuwa na mkutano mzuri sana baada ya huu? [“Amina.”] Tulimshukuru Mungu kwa ajili ya mkutano mzuri sana, sasa tutakuwa na mkutano mzuri sana. Wote wanaoamini hivyo, semeni, “Amina.” [“Amina.”]

Yesu kwa imani,
Na kutumaini (hebu tumwangelie Yeye sasa)
Peke Yako;
Nisikie sasa,
Na kunitakasa,
Ni wako kabisa
Tangu leo!
Hapa nazunguka,
Katika mashaka
Na matata
Palipo na giza
Utaniokoa
Hivi nitaweza
Kufauata.

²⁵⁵ Amina! Kusanyiko lilisema, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.” —Mh.] Haleluya!

Loo, msifuni,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;
Mpeni sifa enyi watu wote,
Kwa maana Damu Yake imeosha kila taka.

Ni zuri jinsi gani!

²⁵⁶ Sawa, hebu tuviinamishe vichwa vyetu sasa kwa dua ya kutakia heri. Sijui ni nani amechaguliwa kufanya hivyo. Ndugu Johnny Manadal, kutoka California, huku tumeviinamisha vichwa vyetu. Sasa msisahau kesho usiku, huo ndio wa kwanza, mwanzo. Kesho usiku, mkutano utakuwa papa hapa, mumu humu kwenye ukumbi huu, saa moja u nusu.

²⁵⁷ Mungu awabariki. Je! mmeufurahia Uwepo wa Mungu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi hebu na tuviinamishe vichwa vyetu huku Ndugu Johnny anapoturuhusu tufumukane.



USIZITEGEMEE AKILI ZAKO MWENYEWE SWA65-0120

(Lean Not Unto Thy Own Understanding)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano, tarehe 20 Januari, 1965 katika Mkahawa wa Ramada kule Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1992 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org